

**MABADILIKO YA LUGHA: HALI MAALUM YA LUGHA YA
EKEGUSII KATIKA ENEO LA GOSETA WILAYANI KWANZA,
KAUNTI YA TRANS- NZOIA**

NA

ABUGA BARNABAS

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI
NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA
CHUO KIKUU CHA MOI
ELDORET**

2013

IKIRARI

Hii ni kazi yangu binafsi na haijwasilishwa kwa shahada ya digrii. Sehemu yo yote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa nakala bila kibali cha mwandishi na / au chuo kikuu cha Moi.

.....

Abuga Barnabas
SASS/PGK/04/06

.....

Tarehe

Tasnifu hii imetolewa ili kutahiniwa kwa kibali chetu kama wasimamizi wa chuo kikuu:

.....
Dkt Issa Mwamzandi
Idara Ya Kiswahili Na Lugha Nyingine Za Kiafrika
Chuo Kikuu Cha Moi

.....
Tarehe

.....
Dkt. Robert Oduori
Idara Ya Kiswahili Na Lugha Nyingine Za Kiafrika
Chuo Kikuu Cha Moi

.....
Tarehe

Tabaruku

Kwa wanangu Olivia Kwamboka, Alvin Omesa na Sammy Abuga na mke wangu mpendwa Jane Omesa bila kumsahau kinara wa kundi la wasaidizi wangu Barack Kinanga.

Shukrani

Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu za kukamilisha kazi hii. Ninawashukuru wasimamizi wangu kwa kunielekeza ilivyofaa hadi nikafuzu.

Nawashukuru pia wahadhiri walionifunza taaluma mbali mbali katika kozi hii. Vile vile nawashukuru wanafunzi wenzangu Kemboi Keitany, Suleiman Amboka, Jacob Savatia, Angela Sawe, Simon Masibo na Ruth Gacengeci kwa michango na himizo zao. Hatimaye nawashukuru wale wote walioshiriki katika kuiwezesha kazi hii kufaulu- watafitiwa, wapiga chapa na wataalamu wote walionipa ushauri.

Mungu awabariki.

ABSTRACT

The study focused on lexical changes and attendant morphological transformations that have occurred with respect to the variety of the Gusii language spoken by the migrant Gusii community of Goseta settlement scheme of Trans-Nzoia County in Kenya. Goseta is one of several settlement schemes in the county that are predominantly occupied by Ekegusii speaking people who migrated from their ancestral homeland in Kisii and Nyamira Counties in the late sixties and early seventies. The study was based on the hypothesis that there are two varieties of the language in existence in the community of study and that they would differ especially on the lexical level given the environmental and other differences between Goseta and the Ekegusii speaking homeland of the respondents in the study. It was supposed that these differences would cause changes in the language as spoken by the respondents. These changes form the focus of this study. The research was conducted as a dialectical survey within the framework of the uniformitarian theory of Language Change and the Social Impact Theory. It entailed collection of data from among Ekegusii speaking residents of Goseta divided into two samples comprising of 50 people. The first sample comprised of 40 Ekegusii speakers aged 10- 40 who were born and brought up in Goseta. The second sample comprised 10 older speakers aged 50 and above who were born in the then Kisii District and migrated to Goseta in the late nineteen sixties and early seventies. Data was gathered using interviews, questionnaires and observation and duly recorded and analyzed for the purpose of compiling this report. In the findings, thus detailed, lexical changes were recorded as having taken place among respondents who were born and raised in the research area. The said lexical changes were accompanied by morphological transformations accruing from the lexical elements identified during the study. The study findings show that the Ekegusii language is rapidly evolving away from the original language spoken by other speakers elsewhere because of the interplay between linguistic, social and economic factors. Ultimately, the changes identified form the basis for concluding that the variety of Ekegusii spoken is an emerging dialect of Ekegusii unique to the area studied. The study recommends further research on the state of the language as spoken in the diaspora.

IKSIRI

Utafiti huu ulidhukuru mabadiliko ya kileksia na michakato ambatani ya kimofolojia mintarafu ya lugha ya Ekegusii inayozungumzwa na jamii ya Abagusii iliyolowea katika eneo la Goseta katika Kaunti ya Trans-Nzoia nchini Kenya. Eneo la makaazi la Goseta ni mojawapo ya maeneo katika kaunti ya Trans-Nzoia ambayo wanajamii wa Abagusii wameilowea. Wanajamii-lugha hawa wa Abagusii walihamia Kaunti ya Trans-Nzoia mnamo miaka ya elfu moja mia tisa sitini na elfu moja mia tisa sabini kutoka eneo la asili katika Kaunti za Kisii na Nyamira kusini magharibi mwa nchi. Nadharia tete iliyoongoza utafiti huu ilichukulia kuwa pangeibuka mabadiliko kati ya launi ya Ekegusii inayozungumzwa miongoni mwa watafitiwa kutokana na tofauti za kimazingira na nyinginezo zilizopo kati ya eneo la utafiti na eneo asili walikotoka watafitiwa. Ilichukuliwa kuwa tofauti hizi zingethiri lugha na kuwa msingi wa mabadiliko. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya usare na ile ya taathira za kijamii. Ulikuwa wa aina ya utaala wa kilahaja uliojumisha ukusanyaji wa data kutoka kwa watafitiwa 50 waliogawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza lilikuwa la watafitiwa 40 wa umri wa miaka ya kati ya 10 na 40 kwa upande mmoja na la pili lilikuwa la watafitiwa 10 wenye umri wa zaidi ya miaka 50. Data ilikusanywa kupitia uchunguzi nyanjani na pia kupitia hojaji, na dodoso mahsusi na kutumika kwa minajili ya kuandika tasnifu hii. Utafiti huu unabainisha kuwa mabadiliko ya kileksia yametokea katika launi tafitiwa na kuibua michakato mahsusi ya kimofolojia inayonakiliwa katika tasnifu hii. Mabadiliko haya ilibainika yalishinikizwa na mseto wa maswala ya kiisimu, kijamii na kiuchumi. Ni matokeo haya ambayo yanapelekea uamuzi kuwa yawezekana kuainisha launi hii ya Ekegusii kama lahaja inayoibukia ya lugha ya Ekegusii ambayo ni maalum mintarafu ya eneo la utafiti. Hatimaye, kunapendekezwa utafiti zaidi kuhusu hali ya lugha hii katika maeneo yenye wingi wa wanajamii ya Abagusii waliyo nje ya eneo lao la Gusii.

Vifupisho vifuatavyo vimetumika katika yasnifu hii:

<i>Mh</i>	-	Mhariri
<i>wah</i>	-	Wahariri
<i>ktk</i>	-	Katika
<i>n.w</i>	-	Na Wenzake
<i>TY</i>	-	Tafsiri Yangu

YALIYOMO

IKIRARI.....	i
Tabaruku.....	ii
Shukrani.....	iii
ABSTRACT.....	iv

IKSIRI.....	v
Orodha ya Vifupisho.....	vi
YALIYOMO.....	vii
Orodha ya Majedwali.....	ix
SURA YA KWANZA.....	1
MISINGI YA UTAFITI.....	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli.....	1
1.2 Suala la Utafiti.....	3
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	3
1.4 Nadharia Tete.....	4
1.5 Umuhimu Wa Utafiti.....	5
1.6 Upeo Wa Utafiti.....	5
1.7 Misingi ya Nadharia.....	6
1.8 Hitimisho.....	11
SURA YA PILI.....	12
YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....	12
2.0 Utangulizi.....	12
2.1 Dhana ya Mabadiliko ya Lugha.....	12
2.1.1 Dhana Ya Leksia.....	15
2.1.2 Neno Ni Nini?.....	16
2.1.3 Mabadiliko Katika Neno.....	20
2.1.4 Aina za Mabadiliko ya Kileksia.....	21
2.1.4.1 Analojia.....	22
2.1.4.2 Etimolojia ya Kitamaduni (<i>folk etymology</i>).....	24
2.1.4.3 Ukopaji.....	24
2.1.4.4 Kubuni Maneno Mapya.....	28
2.1.4.5 Unururishaji Wa Maana Ya Neno.....	29
2.1.4.6 Udondoshaji Wa Maana.....	30
2.1.4.7 Utowekaji.....	30
2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mofolojia.....	31
2.2.1 Uainishaji wa Lugha ya Ekegusii Kimofolojia.....	32
2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Lahaja.....	34
2.4 Hitimisho.....	36
SURA YA TATU.....	37
MBINU ZA UTAFITI.....	37
3.0 Utangulizi.....	37
3.1 Eneo La Utafiti.....	37
3.2 Watafitiwa.....	37
3.3 Uteuzi wa Sampuli.....	38
3.4 Ukusanyaji wa Data.....	39
3.5 Zana za Utafiti.....	40
3.6 Uchanganuzi wa Data.....	41
3.7 Hitimisho.....	42
SURA YA NNE.....	43
MABADILIKO YA KILEKSIA MINTARAFU YA LUGHA YA EKEGUSII	
GOSETA.....	43
4.0 Utangulizi.....	43
4.1 Ukopaji.....	43
4.1.1 Mambo Yaliyopelekea Ukopaji.....	48
4.2 Ufupishaji Wa Maelezo Katika Mazungumzo Au Matamshi.....	49
4.3 Mabadiliko Yaliyotokana na Upanuzi wa Maana za Maneno.....	53
4.4 Udondoshaji wa Maana.....	53
4.5 Mabadiliko Ya Kileksia Mintarafu Ya Nadharia.....	54

4.6	Hitimisho.....	57
	SURA YA TANO.....	58
	MIFANYIKO YA KIMOFOLAJIA.....	58
5.0	Utangulizi.....	58
5.1	Mofolojia Ya Vipashio Vipya Katika Lugha Ya Ekegusii.....	58
5.2	Tathmini Ya Mifanyiko Ya Kimofolojia Katika Lugha Ya Ekegusii.....	64
5.3	Uchanganuzi Wa Mifanyiko Ya Kimofolojia.....	64
5.3.1	Nyanjani.....	64
5.3.2	Kwa Misingi Ya Kinadharia.....	65
5.4	Hitimisho.....	66
	SURA YA SITA.....	67
	UCHANGANUZI WA SABABU ZA MABADILIKO YA KILEKSIA	
	MINTARAFU YA LAUNI YA EKEGUSII INAYOTUMIKA GOSETA.....	67
6.0	Utangulizi.....	67
6.1	Sababu Zilizopelekea Mabadiliko Ya Kileksia Kutokea.....	67
6.1.1	Elimu.....	68
6.1.2	Ujozi Na Wingi Lugha.....	70
6.1.3	Ubadilishaji Msimbo.....	72
6.1.4	Dhima Ya Lugha Ya Ekegusii.....	72
6.1.5	Mitagusano.....	74
6.1.6	Sababu Za Kiuamilifu.....	75
6.1.7	Sababu Za Kimazingira.....	76
6.1.9	Sababu za Kiisimu.....	79
6.1.10	Idadi Ya Watumiaji Lugha.....	80
6.1.11	Utengano.....	81
6.2	Hitimisho.....	82
	SURA YA SABA.....	83
	HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	83
7.0	Hitimisho.....	83
7.1	Mapendekezo.....	86
	MAREJELEO.....	88
	VIAMBATISHO.....	91
	KIAMBATISHO 1: HOJAJI.....	91
	HOJAJI.....	91
	KIAMBATISHO 2: DODOSO LA KWANZA.....	95
	KIAMBATISHO 3: DODOSO LA PILI.....	97

Orodha ya Majedwali

Jedwali 1: Makundi ya Ngeli za Nomino za Ekegusii.....	UK 33
Jedwali 2: Tarakimu za Viwango vya Elimu Miongoni mwa Watafitiwa.....	UK 68
Jedwali 3: Idadi ya Waliojifunza Lugha ya Ekegusii Rasmi.....	UK 69
Jedwali 4: Tarakimu za Ujozi/Wingi Lugha.....	UK 71
Jedwali 5: Mawanda ya Matumizi ya Ekegusii.....	UK 73

SURA YA KWANZA MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii ya kwanza inatoa inatoa usuli wa utafiti kwa kuangazia watafitiwa na lugha tafitiwa. Hali kadhalika inaweka wazi suala la utafiti na upeo ambamo utafiti ulijikita. Imeanisha malengo ya utafiti, na nadharia tete na mikabala ya kinadharia iliyouongoza utafiti wenyewe.

1.1 Usuli

Utafiti huu ulidhukuru mabadiliko ya kileksia na michakato ambatani ya kimofolojia ambayo imejitokeza katika launi ya Ekegusii inayozungumzwa na wanajamii-lugha wa Abagusii wanaoishi eneo la Goseta wilayani Kwanza katika Kaunti ya Trans Nzoia. Lugha ya Ekegusii, ambayo ni lugha ya kibantu, inazungumzwa na jamii ya Abagusii inayopatikana katika vilima vya kusini magharibi mwa Kenya katika Kaunti za Kisii na Nyamira.

Wanajamii ya Abagusii wanaopatikana Goseta walihamia huko mnamo miaka ya sitini na sabini. Walihama kutoka kaunti za Kisii na Nyamira kwa minajili ya kutafuta mashamba ya kuendeleza shughuli za kilimo na ufugaji. Uhamiaji huu ulisababishwa na ukosefu wa ardhi ya kutosha katika Kaunti ya Kisii kutokana na msongamano mkubwa wa watu.

Hivi sasa, wanajamii hawa wanapatikana sehemu mbalimbali za Kaunti ya Trans Nzoia katika maeneo ya mashambani kama vile Nyabomo, North Kisii, Chisare, Nyakoigwana, Gesarate, na Ngorera. Nje ya Kaunti hii wanajamii hii ya Abagusii hupatikana katika Kaunti za Nakuru, Uasin Gishu, Narok na katika miji mbali mbali humu nchini.

Eneo la utafiti la Goseta lililowewa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1969. Idadi ya Abagusii waliolowea hapo ilikuwa 140. Hivi sasa kwa mujibu wa hesabu za idara ya tarakimu wilayani Kwanza, idadi hii imeongezeka hadi kufikia watu 1298. Eneo hili la Goseta linapatikana takribani kilometa kumi mashariki mwa mji wa Kitale ambao ndio mji mkuu wa Kaunti ya Trans Nzoia. Eneo lenyewe

limezingirwa na maeneo mengine yaliyoloewa na watu kutoka jamii tofauti za humu nchini. Maeneo haya ni kama vile Emoru la watu wa asili ya Kiturkana, Amuka la jamii ya Wabukusu na maeneo ya Taito na Kipkorion yenye watu wa asili ya Kikalenjin.

Mbali na Goseta, jamii ya Abagusii inapatikana katika maeneo mengine sita ya kiulowezi katika kaunti hii ya Trans Nzoia ambayo ni Nyabomo, North Kisii, Nyakoigwana, Chisare, Gesarate, na Ngorera. Uteuzi wa eneo la Goseta unakusudiwa kuwakilisha hali ilivyo katika mashamba mengine wanamoishi wanajamii hawa kwenye Kaunti hii.

Swala la mabadiliko ya lugha linaibuka pale inapobainika kuwa launi ya Ekegusii itumikayo na vizazi vilivyozaliwa na kukua katika eneo hili la Goseta ina tofauti zinazojidhihirisha ilinganishwapo na launi ya Ekegusii inayozungumzwa na wenzao waliohamia eneo hili kutoka Gusii kama vile wazazi wao.

Hali hii imetangulia kutajwa na Camenga (2002) ingawa haikutafitiwa ili kudhihirisha mabadiliko yaliyojitokeza. Hata hivyo, Camenga ametaja utengano baina ya Abagusii waishio Gusii na wale waishio nje kuwa kisababishi kikuu cha tofauti zilizopo. Licha ya hayo, hatoi ithibati zaidi za hali hii kwani utafiti aliofanya kuhusu lugha hii ulijikita katika wilaya ya Kisii pekee yake.

Utafiti huu basi ulilenga kutoa mchango kuhusu hali ya lugha hii kwa kuangazia launi ya lugha ya Ekegusii kinachotumika nje ya kaunti za Kisii na Nyamira, kwa kuzingatia eneo la Goseta wilayani Kwanza kwenye kaunti ya Trans Nzoia. Uchunguzi uliofanywa ulilenga vipengele vya kileksia na michakato ya kimofolojia iambatanayo na mabadiliko yo yote yale ya kileksia

Utafiti uliongozwa na nadharia mbili yaani ile ya taathira za kijamii (*social impact theory*) na ile ya usare (*uniformitarian approach*). Utafiti wenyewe ulijumuisha ukusanyaji wa data ghafi moja kwa moja kutoka nyanjani kwa kutumia mbinu kama vile hojaji, dodoso na uchunguzi nyanjani.

1.2 Suala la Utafiti

Wanajamii ya Abagusii wamehamia sehemu mbali mbali nje ya eneo lao la asili la Gusii ambapo wameselea na kuendeleza maisha yao ya kawaida. Katika maeneo haya wamekumbana na tajriba tofauti ngeni hali ambayo bila shaka imeathiri sio tu mahusiano yao ya kijamii bali pia lugha wanayoitumia. Tafiti zilizofanywa na baadhi ya wataalamu kama vile Whiteley (1956, 1959, 1960, 1974) na Camenga (2002) kuhusu mabadiliko ya lugha ya Ekegusii zimelenga maeneo asili ambako lugha hii inazungumzwa. Hususan tafiti hizo zimelenga Kaunti za Kisii na Nyamira ambako vizalia asili wa lugha hii hupatikana.

Hivyo basi, kuna haja ya kufahamu pia jinsi lugha hii inavyochukua maumbo tofauti kwa baadhi ya wanajamii ya Abagusii ambao wanaishi nje ya maeneo yaliyotajwa. Utafiti huu unajaza pengo hili kwa kutafiti mabadiliko ya kileksia na mifanyiko ambatano ya kimofolojia katika lugha ya Ekegusii kama inavyozungumzwa na Abagusii wanoishi eneo la Goseta katika Kaunti ya Trans Nzoia.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kudhukuru mabadiliko yaliyotokea katika lugha ya Ekegusii inavyozungumzwa na wakazi wa eneo la Goseta wilayani Kwanza. Utafiti ulizingatia mabadiliko ya kileksia na michakato ya kimofolojia iambatanayo na mabadiliko hayo ya kileksia. Katika kuafikia madhumuni haya, malengo yafuatayo yalizingatiwa:

- i. Kubainisha mabadiliko ya kileksia yaliyoibuka katika launi ya Ekegusii inayotumika Goseta.
- ii. Kuainisha mifanyiko ya kimofolojia iambatanayo na mabadiliko ya kileksia yanayojitokeza katika launi ya Ekegusii inavyozungumzwa Goseta
- iii. Kuchunguza sababu za kijamii, kimazingira na nyinginezo zinazopelekea mabadiliko ya kileksia yaliyoibuka katika launi ya Ekegusii inayotumika

Goseta.

- iv. Kuweka misingi ya kileksia ya kutambua iwapo launi ya Ekegusii inayotumika Goseta ni mfano mojawapo wa lahaja za Ekegusii.

1.4 Nadharia Tete.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete kuwa;

- i. Launi ya Ekegusii izungumzwayo Goseta na vizazi vilivyozaliwa na kukulia huko inasheheni mabadiliko mengi ya kileksia na kimofolojia ilinganishwapo na ile ya vizazi vya awali ambavyo vilihamia kule kutoka Gusii.
- ii. Sababu za kijamii, kijiografia na kimazingira ndizo zinachangia mabadiliko ya kileksia na kimofolojia katika launi ya Ekegusii inayozungumzwa Goseta zaidi ya umbali na mpito wa wakati
- iii. Mabadiliko ya kileksia yanayotokea yamepelekea kufifia kwa baadhi ya msamiati asili, kuibuliwa kwa msamiati mpya ama kuathirika kwa fahiwa za misamiati iliyopo
- v. Launi ya Ekegusii inayozungumzwa Goseta ni mfano wa lahaja ibuka ya lugha ya Ekegusii

1.5 Umuhimu Wa Utafiti

Utafiti ulivyokusudiwa unatazamiwa kuchangia tafiti nyingine zilizofanywa na wachunguzi mbali mbali kwa kuzingatia hali ya lugha ya Ekegusii nje ya mipaka ya maeneo inapozungumzwa na wengi kule Kisii na Nyamira. Kwa kufanya hivi, utafiti huu unatarajiwa kupanua mawanda ya uchunguzi wa lugha hii.

Vile vile unatarajiwa kuchochea na kuchangia utafiti kuhusu lugha za asili za humu nchini katika mazingira ya kisasa ambapo utandawazi umekita mizizi.

1.6 Upeo Wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika eneo la Goseta wilayani Kwanza. Eneo hili ni

mojawapo kati ya maeneo mengine sita katika kaunti ya Trans Nzoia yaliyo na idadi kubwa ya Abagusii yaani Nyabomo, Chisare, North Kisii, Nyakoigwana, Gesarate, na Ngorera. .

Uteuzi wa eneo la Goseta uliongozwa na sababu ya kuwa eneo lenyewe linafikika kwa urahisi. Vile vile idadi kubwa ya wakazi wake ni Abagusii na hutumia Ekegusii katika mawasiliano ya kila siku miongoni mwao. Isitoshe, mimi binafsi naielewa lugha husika jambo ambalo liliniwezesha kuchunguza suala la utafiti kikamilifu.

Utafiti ulizingatia makundi mawili ya watafitiwa. Kundi la kwanza lilikuwa kundi lengwa la utafiti huu na lilijumuisha watafitiwa wale watu waliokuwa kati ya umri wa miaka 10 na 40. Watafitiwa hawa wamezaliwa na wamekulia eneo la Goseta tangu utotoni. Hivyo basi wamejifunzia lugha huko na wala sio katika Kaunti za Kisii na Nyamira. Vile vile wanawakilisha kizazi cha sasa na wamepokea elimu rasmi shuleni. Watafitiwa hawa walikuwa wa kiume pamoja na wa kike, na ambao wazazi wao wawili ni wazungumzaji wa lugha hii. Kundi la pili lilijumuisha kizazi kile cha awali kilichohamia eneo hili la Goseta mnamo miaka ya sitini na sabini. Wanakundi hili ambao umri wao ulikuwa zaidi ya miaka 50 walikuwa wamejifunza lugha ya Ekegusii katika mazingira tofauti kule walikotoka na hivyo basi walikuwa na kiwango tofauti cha ujuzi wa lugha hii. Kundi hili la pili ndilo lilitarajiwa kuyakinisha matokeo ya utafiti kwa kuwa msingi wa ulinganishaji wo wote uliufanywa.

Utafiti ulijikita katika uchunguzi wa mabadiliko ya lugha kwa kuzingatia mabadiliko ya kileksia yanayoathiri maneno katika lugha hii. Ulitazama jinsi ambavyo maneno mbali mbali yamepanuliwa kimaana, mengine kubanwa kimaana kwa kule kuelezea dhana finyu zaidi, na mengine yakatoweka huku mengine mapya yakijumuishwa katika lugha.

Mbali na mabadiliko ya kileksia, utafiti ulichunguza mifanyiko ya kimofolojia iliyoambatana na mabadiliko ya kileksia yaliyoshuhudiwa kwa minajili ya kubainisha

iwapo maumbo ibuka yataidumu katika lugha hii au ni ya muda tu.

Uteuzi wa vipengele vya kileksia na kimofolojia uliongozwa na uwezekano wa kupata data inayoweza kukusanywa, kuhakikiwa na kutathminiwa kwa wepesi katika kipindi cha kufanya utafiti.

1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili. Nadharia ya kwanza ni ile ya usare ambayo ni nadharia iliyoasisiwa na Leskien, Brigman na Osthof (*ktk Davies 1994*). Nadharia hii ilisisitiza ya kuwa mabadiliko ya lugha hutokea kwa njia sawa katika lugha yoyote ile. Misingi wa mabadiliko haya ya lugha ni mabadiliko katika matamshi ya maneno.

Wananadharia hii wanaendelea kufafanua kuwa mabadiliko haya huzingatia mifanyiko ya kianalojia yanapotokea. Kulingana nao watumia lugha wanapoipokea lugha hawarudii moja kwa moja maumbo yale yale waliyoyapata bali huibuka na maumbo mapya wakiongozwa na miundo iliyopo tayari. Hali hii inapokita mizizi ndio hupeleka kuibuka kwa maumbo mapya ya kileksia. Hoenigswald (1960) anataja misingi miwili ya kutokea kwa mabadiliko ya kileksia yaani:

Ukongwe – pale ambapo neno linasita kuwa na uamilifu wo-wote kwa watumia lugha kutokana na mpito wa wakati na pia kutokana kubadilika kwa mazingira ambamo neno hilo lilikuwa na uamilifu.

Upya – pale ambapo neno jipya huibuliwa ili kuelezea hali ngeni iliyotokea.

Katika hali zote mbili mabadiliko ya kileksia husemekana kutokea na hivyo basi mabadiliko ya lugha.

Hock na Joseph (1996:292) wakichangia nadharia hii ya usare walidai kuwa mabadiliko yanapozuka yawe ni ya kifonolojia, kimofolojia au kisemantiki katika lugha hatimaye hutambulika tu kama mabadiliko ya kileksia.

Joseph (1999) anadai kuwa nadharia hii inasisitiza ya kwamba mabadiliko ya kileksia ndiyo dhihirisho kuu la kutokea kwa mabadiliko ya lugha. Mabadiliko hayo

hata hivyo, alidai, sharti yatambulike na kukubalika na wanajamii wote ndipo yakaweze kuainishwa kama madhihirisho thabiti ya mabadiliko ya kileksia. Hivyo alipendekeza kuwepo kwa kanuni sare zinazotawala na kuyaongoza mabadiliko katika lugha hadi yakakubalika kuwa sehemu ya lugha husika.

Kanuni hizi anazitaja kama zifuatazo:

i. Makusudi

Mabadiliko sharti yanuie kutimiza makusudi fulani maalum. Mathalani kujaza pengo linalotokana na ukosefu wa neno mwafaka la kuelezea dhana fulani. Hali hii itapelekea wanajamii – lugha husika kuhalalisha neno jipya au mabadiliko katika umbo la neno hilo ili kuafikia malengo yao maalum ya kimawasiliano.

ii. Uhawilishaji

Neno jipya sharti lilingane kadiri inavyowezekana na mfumo bia wa lugha husika kiasi cha kuweza kudhihirika kama sehemu ya lugha hiyo. Hali hii katika baadhi za lugha kwa mfano hupelekea uambishaji wa neno.

iii. Uamilifu

Neno jipya litakubalika na kudumishwa kama sehemu ya lugha husika endapo litatosheleza dhima kuu ya neno yaani kule kuelezea dhana husika barabara.

iv. Tathmini

Licha ya kukubalika neno au umbo jipya hukadiriwa mara kwa mara mintarafu ya majukumu lililonuiwa kuyatekeleza. Endapo litadhihirika kuwa pungufu, si nadra kwalo kusita kutumiwa. Iwapo linafaa, basi litaenea miongoni mwa jamii pana.

v. Uenezaji

Uenezaji wa neno au umbo jipya utafanyika kwa haraka miongoni mwa wanajamii watumia lugha pale inapong'amuliwa kuwa hamna kipingamizi chochote dhidi ya matumizi yake katika mawasiliano ya kawaida baina ya wazungumza lugha.

Vinginevyo, kwa mujibu wa nadharia hii, mabadiliko hayatokei kwa ghafla bali ni

jambo linalotokea hatua kwa hatua. Isitoshe jamii itumiayo lugha ndiyo hudhibiti mwelekeo wa mabadiliko husasan iwapo yatadumu au la.

Nadharia ya pili iliyoitumika ni ile ya taathira za kijamii ambayo ina asili ya taaluma ya saikolojia jamii. Nadharia hii iliasisiwa na Bibi Latané mnamo mwaka wa 1981 kwa lengo la kutoa mwongozo wa kinadharia ungalioelezea jinsi imani, tabia, mienendo, maadili, itikadi, tamaduni, motisha na hata ujuzi alio nao mtu binafsi unavyoathiriwa na mtagusano baina yake na wajamii wenzake. Alidai kuwa mitagusano hii hupelekea taathira mbali mbali alizojiita taathira za kijamii.

Nowak (1990) alibaini uwezekano wa kuitumia nadharia hii katika kuelezea mabadiliko ya lugha. Alidahili kuwa lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii - haswa mojawapo kati ya sifa pambanuzi za utamaduni wa jamii. Kulingana na ufafanuzi wake sifa pambanuzi za utamaduni wa jamii ni jumla ya mambo ambayo wanajamii hupokezana kwa kufunzana. Kwa vile lugha hupokezwa baina ya wanajamii kwa kufunzana, basi ilitosha kutazamwa sawia na sifa pambanuzi nyingine za utamaduni wa jamii na hivyo basi kuchunguzwa kwa misingi ya nadharia hii.

Nowak alidai ya kuwa uwasilishaji wa jambo lo lote unaofanywa kupitia mafunzo ya kijamii aghalabu hukumbwa na uwezekano mkubwa wa kuendeleza maumbo yasiyo sahihi kati ya wanajamii. Hivyo basi, alidai si nadra kwa limbuku kujifunza maumbo yaliyo na mushkeli fulani. Hali kadhalika katika mazingira ya wingi lugha ukopaji wa maumbo mageni ni jambo la kutarajika. Matokeo ya harakati hizi zote ni kuibuka na kisha kuenea kwa maumbo mapya kama vile maneno miongoni mwa watumia lugha husika.

Maneno kwa mujibu wa Hudson (1996), yanaathirika jinsi hii kwa vile ni miongoni mwa vile vipashio vya kiisimu ambavyo mtumia lugha anaweza kujifunza binafsi na pia mbali na vipengele vingine vya lugha. Hivyo basi mitagusano baina ya wanajamii hupelekea kuibuka kwa athari ambazo kwa muktadha wa lugha hubainika kama mabadiliko ya lugha.

Nadharia hii inaorodhesha mambo matatu makuu ambayo yanadaiwa kuchagiza na hatimaye kurasimisha mabadiliko katika lugha. Mambo haya ni:

Tofauti za kiushawishi miongoni mwa wanajamii. Nadharia hii yashikilia kuwa katika jamii yo yote ile pana wanajamii walio na ushawishi mkubwa zaidi kuliko wenzao. Ushawishi huu huweza kutokana na uwezo mkubwa zaidi wa kiuchumi, kijamii, kisiasa, kielimu, kidini nakadhalika walio nao wanajamii hao. Matokeo ya hali hii ni kuwa jambo geni linapoasisiwa nao, pana uwezekano mkubwa kwalo kuenea na kuathiri wanajamii wengine. Kuenea huku kutashinikizwa na desturi miongoni mwa wanajamii yo yote ile ya kutaka kujihusisha na wale watu au makundi ya watu wanayoyachukulia kuwa na umuhimu katika kufaulisha mikakati yao anuwai. Hivyo basi endapo kutatokea mabadiliko, asili au chanzo chake ni wanajamii wenye ushawishi mkuu. Katika muktadha wa kazi hii, wao ndio wataibua maneno mapya na kupelekea kuenea kwayo miongoni mwa jamii

Kiwango cha kuzoeana baina ya wanajamii wenye ushawishi na wale wanaopokezwa athari za ushawishi huo. Endapo kiwango hiki ni cha chini, pana uwezekano wa mitagusano kuathiriwa na hivyo basi jambo lo lote geni lingaliloibuliwa kuathirika.

Idadi ya wale walio na uwezo wa kushawishi. Idadi hii ndiyo itafanya jambo jipya kukubalika au kukataliwa.

Hivyo basi mabadiliko ya lugha kwa mujibu wa nadharia hii ni zao la mitagusano baina ya wanajamii. Mitagusano hii ina athari mbali mbali ambazo katika muktadha wa lugha hujitokeza kama mabadiliko katika maneno na maumbo mengineo ya lugha.

Uamilifu wa nadharia hii unadhihirika kwa kutupa mkabala wa kuelezea chanzo cha matumizi ya vipashio vya kileksia ambavyo ni vigeni katika lugha husika kama vile vya mkopo au vinavyotokana na kuchanganya ndimi.

Ni dhahiri kuwa nadharia hizi zinadai ya kwamba mabadiliko ya lugha hayatokei kiholela bali hutawaliwa na maswala mbali mbali. Nadharia,hasa ya taathira za kijamii ni muhimu kwa utafiti huu kwa vile inasisitiza umuhimu wa athari za baadhi wanajamii juu ya wenzao katika kuasisi na kuelekeza mabadiliko ya lugha hususan ya kileksia. Nadharia hii pia ina ufaafu kwa utafiti huu kwa kule kushikilia kuwa mabadiliko hutokea, kuenea na kukita mizizi miongoni mwa kundi dogo la watumia lugha kulio ilivyo katika kundi kubwa. Hali hii ndiyo inatawala katika eneo la utafiti ambapo kundi la wanajamii lugha ni dogo.

Katika sura zifuatazo vipengele vikuu vya nadharia hizi vitajidhihirisha pale ambapo uchanganuzi wa data iliyokusanywa nyanjani utaangaziwa kwa kina ili kubaini ufaafu wa mabadiliko ya kileksia na michakato ambatani ya kimofolojia.

1.8 Hitimisho

Sura hii imetoa habari kuhusu lugha iliyofanyiwa utafiti, wafitiwa na eneo wanomishi. Vilelvile imebainisha suala la utafiti na pia malengo ya utafiti.

Imedhihirika ya kwamba utafiti uliongozwa na mitazamo miwili ya kinadharia ambayo inachangiana na hivyo basi kuufaidi utafiti kwa kuupa msingi imara wa kinadharia.

SURA YA PILI

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

2.0 Utangulizi

Sura hii inajishughulisha na yale yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya kazi.

Inatalii maandishi mbali mbali kuhusu mabadiliko ya lugha kwa ujumla wake na yale ya kileksia kwa undani. Vile vile inaangazia dhana ya mofolojia na jinsi mifanyiko ya kimofolojia inavyoathiri neno. Hatimaye, inaainisha yaliyoandikwa kuhusu lahaja na misingi inayotumika katika kuianisha lahaja mbali mbali za lugha.

2.1 Dhana ya Mabadiliko ya Lugha

Utafiti uliongozwa na welewa kuwa tunapotaja lugha humaanisha mfumo maalum wenye muundo dhahiri unaotawaliwa na kanuni mwafaka. Ilikeleweka kuwa muundo wa lugha unatokana na viamba-jengo mbali mbali. Viamba-jengo hivi ni kama vile sauti, maneno, uundaji wa maneno, fahiwa zinazoambatana na maneno yenyewe na tungo zinazoibuka kutokana na kutumiwa kwa maneno hayo kwa lengo la kuwasilisha ujumbe maalum. (Kembo-Sure na Webb 2000).

Yule (2000) anataja mabadiliko ya lugha kuwa yale yanayoathiri matamshi ya maneno, uundwaji wa maneno hayo na vile vile jinsi yanavyotumika katika tungo ili kuleta maana na hata katika kanuni zinazotawala utumizi wayo katika kuafikia lengo hilo la kuzalisha maana.

De Saussure (katika Bally *n.w* 1969) anasema kuwa mabadiliko ya lugha hutokea pale ambapo uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa unapoathirika. Hali hii husababishwa na umbo la kiashiria kubadilika, dhana inayoashiriwa kubadilika au kiashiria chenyewe kuashiria dhana tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Akifafanua kuhusu nini hasa kinachobadilika katika lugha, Dittmar (1976)

anadai kuwa elementi ambazo hazijajikita ipasavyo katika mfumo thabiti wa muundo wa sarufi ya lugha ndizo hubadilika kwa wepesi zaidi. Mfano wa elementi hizi ni zile za kileksia. Elementi za kisintaksia kwa upande wao hudhihirisha nguvu kinza zaidi dhidi ya mabadiliko.

Coates (2007) akifuatia Labov (1978) anadai kuwa mabadiliko ya lugha huanzia miongoni mwa baadhi ya wanajamii na hatimaye kuenea kwa jamii pana (<http://en.wikipedia.org/wiki/language-change>). Hivyo basi mabadiliko hayawezi kuratibiwa pasi na kukubalika na jamii. Maumbo haya yaliyozuka kutokana na kukubalika huku ndiyo yanayochunguzwa .

Kwa mujibu wa De Saussure (Lodge 1988) kila lugha hubadilika kulingana na wakati na shinikizo za nguvu tendaji za kijamii. Mabadiliko hutokea pale ambapo dhana mpya zinaibuka na pia mahitaji ya jamii dhidi ya lugha yake yanapopanuka na kuipelekea kudai utoshelezwaji zaidi kutoka kwa lugha yenyewe. Kwa maneno yake Yule (2000), mabadiliko yatokeapo katika lugha yo yote kimsingi huakisi uwezo wa mwanadamu dhidi ya lugha yake kwa minajili ya kutekeleza majukumu yake ya kimawasiliano.

Kembo-Sure na Webb (2000) wanadai kuwa mabadiliko husababishwa na utengano baina ya wanajamii lugha moja. Utengano huu waweza kusababishwa na vizuizi vya kimazingira kama vile milima na maziwa. Hali hii hupelekea launi tofauti za lugha moja kuibuka. Launi hizi hubainishwa na maumbo tofauti ya vipengele vyazo, kanuni tofauti zinazotawala matumizi ya vipengele hivyo na hata fahiwa tofauti za maneno. Wametoa mfano wa launi au lahaja tofauti za Kiluo- lugha ya kinailotiki inayo zungumzwa mkoani Nyanza - na launi sawia nacho kama vile Kiacholi na Kipadhola zinazozungumzwa nchini Uganda.

Kamwangamalu (2000) anataja mitagusano baina ya jamii lugha tofauti kuwa inasababisha mabadiliko katika lugha kuzuka. Mitagusano hii husababisha lugha kuathiriana. Hali hii hupelekea ubadilishaji misimbo, daiglossia na pia mabadiliko ya

lugha. Kwa mujibu wake haiwezekani lugha tofauti kutagusana zisiathiriane.

Mabadiliko katika lugha pia huweza kutokana na uhamaji. Fishman (1969) amenakili mifano mbali mbali ya lugha za kienyeji za wahamiaji kule Marekani ambazo zimeathirika na uhamaji zikabadilika. Aghalabu katika hali hizi mabadiliko hushinikizwa na haja ya wahamiaji kutafuta mbinu za kukabiliana na mazingira yao mapya.

Mikakati ya upitishaji lugha baina ya vizazi pia ni chanzo cha kutokea kwa mabadiliko ya lugha. Dai hili linaungwa mkono na wataalamu mbali mbali. MATHALANI Nettle (1999b) anaorodhesha mambo yafuatayo kuwa yenye athari dhidi ya jumla ya michakato ya uwasilishaji lugha baina ya vizazi:

- i. jinsi watoto wanavyokuzwa
- ii. mfumo wa mahusiano baina ya wanajamii
- iii. kiwango cha mitagusano kati ya watu wa makundi mbali mbali katika jamii
- iv. kiwango cha ujozi- lugha au daiglosia miongoni mwa wanajamii
- v. kuwepo kwa miiko ya maneno
- vi. mitazamo na desturi za wanajamii kwa jumla

Naye Yule (2000) anadai kuwa kila kizazi kipya hushurutika kuibua jinsi tofauti za za kuitumia lugha ya kizazi kilichotangulia ili kukidhia mahitaji yake. Matokeo ya juhudi hizi hujidhihirisha kupitia mabadiliko bayana kati ya lugha ya kizazi kilichopo na kile cha awali.

Vile vile, mara nyingi watumia lugha wana mazoea ya kurahisisha mazungumzo ili kufanikisha mawasiliano baina yao. Kwa mujibu wa Barber (2000) hii ni kaida ya lugha inayopelekea kuibuka kwa mabadiliko katika katika lugha husika. Mabadiliko hayo hujitokeza mathalani kupitia ufupishaji wa baadhi ya sauti za maneno. Jambo hili linapokita mizizi, habainika kama mabadiliko katika lugha.

Mabadiliko yanapotokea, lugha huweza kuimarika na kuwa na uamilifu mkuu

zaidi miongoni mwa wanajamii kwa kule kuweza kuyakidhia mahitaji yao kimawasiliano zaidi.

Kwa upande mwingine, mabadiliko huweza kuifisha au kuichakaza lugha. Kwa mujibu wa Myers- Scotton (*ktk Brezinger 1992*) wakati lugha inapoteza uamilifu wake kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa wanajamii, inatoweka. Anadai kuwa hali hii husabababishwa na watumia lugha kukosa udhibiti juu ya lugha yao na hivyo basi kukosa kuipa kipaumbele katika mikakati yao ya kimawasiliano. Kuchakaa nakwo kwa mujibu wa Jurgen-Sasse (*ktk Brezinger 1992*) kunatokana na hali ambapo maumbo ya kileksia yanatoweka au kufifia kimatumizi miongoni mwa watumia lugha. Hali hizi aghalabu hutokea katika mazingira ya wingi lugha – jambo ambalo linazua ushindani baina ya lugha na hatimaye kuibua mabadiliko katika lugha. Mabadiliko haya mara nyingi huwa ya kileksia.

Jumla ya haya yote ni kuwa lugha itabadilika kwa viwango mbali mbali kwa kutegemea mahali na wakati.

2.1.1 Dhana Ya Leksia

Kulingana na kamusi ya Kiingereza-Kiswahili (T.U.K.I.2000) leksia ni “msamiati”. Msamiati katika Kamusi Ya Kiswahili Sanifu (T.U.K.I.1981) ni jumla ya maneno katika lugha. Massamba (T.U.K.I.2000) katika Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha anaelezea msamiati kuwa jumla ya maneno yanayotumika katika lugha. Hivyo basi, tunapotaja leksia tunadhamiria kuashiria maneno yote yanayopatikana katika lugha. Kila lugha ina leksia yake ambayo ni tofauti na ile ya lugha nyingine.

Kwa hali hii basi uchunguzi kuhusu mabadiliko ya kileksia katika lugha, huyadhukuru mabadiliko yanayoathiri maneno ya lugha hiyo - mabadiliko ambayo hatimaye hudhihirika kama mabadiliko katika lugha. Hata hivyo kabla ya kuzamia michakato mbali mbali inayohusiana na mabadiliko ya kileksia, ni muhimu kuangazia dhana ya neno kwanza.

2.1.2 Neno Ni Nini?

Hapana kijezezi cha moja kwa moja cha istilahi “neni”. Hali hii yamkini yatokana na sababu kuwa neno laweza kudhihirika kama herufi au sauti moja tu ama mkururo au mfuatano wa sauti au herufi za idadi fulani – idadi ambayo itategemea lugha husika.

Kulingana na kamusi na ensiklopedia mbali mbali neno hutajwa kama:

- i. “Silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na kuleta maana” (katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI 1981).
- ii. “Kipashio cha usemaji ambacho hujengwa na mwandamano au mkururo wa sauti zilizopangika kisilabi na ambazo hutambuliwa na wasemaji wa lugha inayohusika na wasemaji kuwa kitu kimoja chenye maana mahsusi.” (Katika Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha (Massamba 2004).
- iii. “Kipashio cha lugha kibebacho maana na ambacho kinajumuisha mofimu moja au zaidi zilizounganishwa pamoja. (Katika *Encyclopedia of Language and Linguistics* (Brown 2005).

Kinachojitokeza kwa haya maelezo yote ni kuwa neno lina umbo, muundo na maana. Hali hii hasa ya kuwa na maana hulipa neno uzito mkubwa zaidi pale inapozingatiwa kuwa ni kutokana na uwezo huu wa kubeba maana ambapo mawasiliano kati ya watumia lugha hutimia.

Maneno huchukuliwa kwa namna mbali mbali na wataalamu tofauti matahalani kwa wanaisimu nafsia maneno ni misimbo au viashiriaji vya miundo ya maarifa: ndilo dhihirisho bayana la kuwepo kwa wazo au dhana fulani.

Miongoni mwa wanaisimu, neno huchukuliwa kwa upande mmoja kama kipashio kidogo zaidi cha kisintaksia. Ndilo msingi wa umbo lo lote lile la kisintaksia. Kimofolojia, neno ndilo kipashio kikubwa zaidi. Katika mwelekeo huu, neno

husemekana kutokana na mofimu moja au mseto wa mofimu kadha Mseto huu wa mofimu huibua leksimu ambayo ni kipashio cha kidhahania cha uchanganuzi wa kimofolojia katika lugha. Dhana ya leksimu huongozwa na kauli kuwa neno moja huweza kuchukua maumbo tofauti kuelezea mambo mbali mbali. Hivyo basi, leksimu ni sawa na jumla ya maumbo yote yanayoweza kuchukuliwa na neno moja (Crystal 1995).

Massamba (2004) anataja leksimu kuwa kipashio kidogo zaidi cha upambanuzi cha kileksia katika mfumo wa semantiki ya lugha. Istilahi hii anadai ilichombezwa na kuwepo kwa haja ya kuondoa utata unaojitokeza katika matumizi ya faridi “neno” kurejelea viwango vya otografia, fonolojia, sarufi na kileksika.

Neno leksimu linapotumika hurejelea maana ambayo ni dhahania zaidi na ambayo inahusu zaidi msamiati wa lugha husika. Leksimu zina sifa zifuatazo:

- Hulingana na kategoria maalum za kiisimu
- Kila leksimu ina maana maalum
- Miongoni mwa lugha zenye unyambulikaji (*agglutinative languages*), leksimu huchukua maumbo mengi tofauti

Mbali na vijejezi hivi, wanaisimu mbali mbali wametoa maelezo zaidi kuhusu dhana ya neno

Ferdinand De Saussure (*ktk Bally 1959*) anatambua neno kuwa ni ishara ya kiisimu. Anadai kuwa kila neno ni ishara ambayo huashiria dhana fulani mahsusi. Pasipo na kile kinachoashiriwa, basi ishara itakosa uamilifu wa kiisimu (Bally 1959).

Kulingana na De Saussure, kile kinachowasilishwa na neno kina asili yake katika akili ya mtumia lugha. Neno basi hukipa umbo dhahiri kitu hiki kilicho zuliwa akilini mwa mtumia lugha kimaandishi au kiamatamshi. Kile kinachobuniwa akilini ni dhana.

Uhusiano baina ya umbo hili lililotamkwa au kuandikwa na litajwalo kama neno na dhana linaloisimamia adai De Saussure ni wa kinasibu au kiholela tu. Maanake hamna uhusiano wa moja kwa moja baina ya neno na kile ambacho neno hilo linawakilisha kupitia matamshi au maandishi(*ktk Bally 1959*). Hii ndiyo sifa ambayo De Saussure anaitaja kama “sifa ya uholela ya ishara” (*arbitrariness of the sign*). Sifa hii ya uholela wa ishara ya kiisimu ndio chanzo cha kuweko kwa maneno tofauti katika lugha mbali mbali yanayoelezea dhana ile ile moja.

Kauli hii hata hivyo hukiukwa panapo maneno ya kionomatopea na pia vihisishi. Katika mifano hii, kwa kiasi fulani pana uhusiano wa moja kwa moja baina ya neno na ile dhana inayowasilishwa nalo. Zingatia mifano kama vile:

- Alilia wuuui wuuui!
- Gunia lilianguka tiff!
- Alimpiga puu!

Katika mifano hii, maneno yaliyopigwa mstari hulingana na dhana inayowakilishwa na kitendo husika yaani kulia, kuanguka na kupiga.

Neno kwa maelezo ya De Saussure lina sifa mbali mbali. Kwa mfano anadai kuwa neno lina sifa ya utobadilikaji (*immutability*) kwa upande mmoja na ubadilikaji (*mutability*) kwa upande mwingine.

Neno husemekana kuwa lina sifa ya utobadilikaji kwa vile hamna mtumia lugha binafsi anayeweza kulibadili na lingine katika lugha hiyo hiyo moja. Hii ni kutokana na sababu kuwa hamna sababu ya kimantiki au yenye umaalum iliyo pelekea kuteuliwa kwa neno hilo kuwakilisha dhana linaloiwakilisha na kwa hivyo pia hamna msingi wo wote wa kulibadilisha.

Isitoshe lugha hutumika kwa wakati mmoja na watu tofauti walio sehemu tofauti jambo linaloondolea mbali uwezekano wa kuwepo na uwiano baina yao kuhusu kubadilisha sehemu yo yote ila wanuie kuvuruga mawasiliano miongoni mwao (1959). Kwa maana nyingine, mtumia lugha mmoja akitaka kuzua mabadiliko

yanayoathiri kipengee cho chote kile cha lugha yake, sharti awe na sababu maalum inayokubalika na watumia lugha wote kwa wakati moja - jambo lisilowezezana.

Hali kadhalika, neno ni sehemu ya lugha na daima lugha ni mirathi ya kipindi kilichotangulia kwa kizazi kilichopo. Kutokana na ukweli huu, ishara zote, kanuni zote na sifa nyinginezo za lugha hupitishwa kwa kizazi kinachofuatia pasipo na uamuzi wa kizazi hicho kipokezaji kuhusu kile kitakachokubaliwa au kukataliwa. Kwa maneno mengine, watumia lugha hawana uamuzi wote ule kuhusu lugha waitumiayo bali wao huipokea tu.

Vinginevyo basi, ni dai la De Saussure ya kuwa hali fulani ya lugha ni zao la nguvu na michakato ya kihistoria. Nguvu hizi ndizo zinazotawala na kuidhibiti lugha kiasi kuwa ishara zake haziwezi kubadilika kiholela.

Zaidi ya hayo, watumia lugha wa kawadia hawana ufahamu razini kuhusu kanuni zinazoitawala lugha wanayoitumia. Kwa hivyo, ni muhali kupata kuwa wamejitwika jukumu la kuibadilisha kwa vyo vyote vile. Badala yake, wao huridhika na jinsi lugha ilivyo.

Kwa upande mwingine de Saussure alidai ya kuwa ishara ya kiisimu, yaani neno ina sifa ya ubadilikaji. Hali hii hutokana na uwezo wa hii ishara kujiendeleza yenyewe. Kwa sifa hii, mifumo ya awali ya kiisimu hudumu kwa muda mrefu na kwa sababu ya kudumu kwao mifumo hii hubadilika.

Mabadiliko yanapotokea yanaathiri uhusiano baina ya ishara na kiashiriwa. Mara nyingi, hamna lugha yoyote iwezayo kustahimili nguvu zinazoathiri uhusiano huu.

Mabadiliko ya ishara ya kiisimu yatokeapo hushinikizwa na maswala matatu yafuatayo:

- i. Lugha yenyewe
- ii. Watumia lugha

iii. Mpito wa wakati

Ni pale maswala haya matatu yanapoingiliana ndipo lugha na hususan ishara ya kiisimu hubadilika.

2.1.3 Mabadiliko Katika Neno

Mabadiliko ya kileksia ni sehemu ya michakato pana ya ubadilikaji wa lugha. Msingi wa mabadiliko haya ni kule kugeuka kwa uhusiano baina ya kiashiriwa na kiashiria. Kwa mujibu wa De Saussure (1959), uhusiano huu husemekana kubadilika pale:

- a) Ishara mpya au ishara tofauti itatumika kuelezea dhana ile ile
- b) Ishara ile ile itatumika kuelezea dhana tofauti
- c) Dhana inapobadilika na hivyo kulazimu kuweko kwa ishara nyingine itakayoielezea

Kwa mujibu wa Joseph (1999) mabadiliko ya kileksia yanapotokea, kunaibuka miundo mipya ya maneno, utamkaji mpya au tofauti wa maneno au panatokea maana tofauti ya maneno.

Uchanganuzi wa yale wanayoyasema wataalamu hawa kimsingi waonyesha kuwiana kimawazo kwa vile wote wanadai kuwa mabadiliko ya kileksia ni mabadiliko ambayo huathiri neno na ile dhana ambayo linawakilisha. Athari hizi hutokea pale:

- i) Neno linachukua umbo jipya huku likiendelea kubeba maana ile ile au
- ii) Maana inayowakilishwa na neno lile itabadilika na hivyo kulipa neno hilo dhima mpya katika lugha au
- iii) Neno lile lile litaacha kuelezea dhana ile ya awali na badala yake kuelezea dhana tofauti.

Mabadiliko ya namna hii kwa mujibu wa de Saussure, ni jambo lisiloweza kuepukika hata lugha iwe madhubuti jinsi gani (Bally 1959). Ni mabadiliko ambayo yanashinikizwa na nguvu zilizo nje ya udhibiti wa mtumia lugha. Nguvu hizi kwa

mujibu wa Blank (1997, 1997a) ni za:

- Kiisimu
- Kisaikolojia
- Kijamii-tamaduni
- Kiada

Kwa namna nyingine, hizi ni nguvu ambazo zinawajumuisha watumia lugha, mazingira ambamo lugha inatumika na lugha yenyewe. Nguvu hizi hupelekea kutokea kwa mabadiliko ya kileksia ya ghafla au hatua kwa hatua.

2.1.4 Aina za Mabadiliko ya Kileksia

Mabadiliko ya kileksia huweza kutokea kwa namna mbali mbali. Wanasarufi mpya wa karne ya kumi na tisa walipendekeza kuwa panapo mabadiliko ya lugha, mabadiliko ya kileksia ni jambo la kutarajiwa sawia na yale ya kifonetiki. Walidai kuwa mabadiliko ya kileksia ni zao la michakato ya kianalojia (Davies1994). Naye Herman Paul (ktk Davies 1994) aliendeleza mawazo haya kwa kudai ya kuwa analojia ndio chanzo sio tu cha maumbo mapya katika lugha bali pia ubunifu ambao hatima yake ni mabadiliko katika lugha (Davies1994).

Mawazo haya yangali yana uzito hata wakati huu wa sasa na wataalam wengi wa kisasa wanataja analojia kama mojawapo wa michakato inayopelekea mabadiliko katika lugha

2.1.4.1 Analojia

Analojia yaweza kuelezwa kama “ile tabia ya kitu kufuata mkondo au sura ya kitu cha aina yake kilichotangulia” (Massamba 2004). Katika muktadha wa kazi hii “kitu” ni neno ambalo husemekana kufuata mkondo wa neno lingine la aina yake lililotangulia au lililopo tayari.

Mabadiliko ya kileksia yanapoongozwa na analojia kwa mujibu wa Hock (1996), husababisha maneno yo yote ambayo yanafanana kwa namna fulani kubadilika kwa mujibu wa sifa zao za kimofonemiki. Vinginevyo kwa mujibu wa

De Saussure (Bally1959) mabadiliko ya kianalojia huathiri umbo la neno yaani kile kiashiriaji.

Msingi wa analojia kudaiwa kuwa mchakato upelekeo kubadilika kwa lugha kileksia ni kwamba iwapo umbo jipya litaingishwa katika lugha kwa njia yo yote ile, sharti litajaribu kulingana na maumbo mengine katika lugha hiyo. Mlingano huu hupitia hatua tatu kwa mujibu wake De Saussure (Bally1959). Hatua hizi ni:

- i. utambuzi wa umbo asili
- ii. kuibuka kwa umbo shindani
- iii. Kuzuliwa kwa umbo mseto ambalo linazingatia sifa za maumbo yote mawili yaani lile asili na lile shindani.

Analojia husemekana kuanza kama tukio la kimazungumzo la kinasibu linaloanzia mzungumzaji mmoja kisha likaenea hadi kwa watumia lugha wengine (1959).

Hali hii kwa mujibu wa Davies (1994) inalingana na madai ya wanasarufi mpya kuwa watumia lugha mara nyingine hawana uwezo wala nia ya kurudia moja kwa moja maumbo wanayoyapokea sisisi bali saa zote wamo mbioni kubuni upya kianalojia maumbo sawia na yale wanayoyapokea.

Uzalishaji wa umbo jipya alidai De Saussure ni jambo linalotokea akilini. Kila mtumia lugha ana huo uwezo. Mabadiliko ya kianalojia yanayodumu hayatokei kwa ghafla bali hutokea baada ya muda mrefu. Kwa kweli, umbo jipya huanzia mtumia lugha mmoja kisha likaenea kwa kuigwa na watumia lugha wengine. Sifa ya maneno kubadilika kianalojia hata hivyo ina mipaka. Kuna baadhi ya maneno ambayo yana sifa ambazo huzuia ubadilikaji kwa jinsi hii na kuna yale ambayo hubadilika kwa urahisi. Kwa mfano, majina ya mahali hayabadiliki kwa namna hii. Hii ni kutokana na sababu ya kuwa elementi zake hazikubalii uchanganuzi na ufasiri wazo kwa urahisi (Bally 1959).

Hata hivyo sio kila neno jipya lililotokana na analojia hukubalika katika lugha. Mara nyingi maumbo mapya hutumika kwa muda mfupi kisha yakatoweka tena.

Maumbo yale machache yatakayodumu ndio hupelekea mabadiliko halisi katika lugha.

Vile vile mabadiliko haya hutegemea lugha hivi kwamba kuna lugha ambazo hukubalia mabadiliko ya kianalojia kwa urahisi zaidi kuliko nyingine. Mabadiliko ya kianalojia yanapokamilika husababisha sio tu mabadiliko ya kipashio cha kileksia bali pia hupelekea uimarishaji wa kundi zima la vipashio vingine husika vya kileksia.

2.1.4.2 Etimolojia ya Kitamaduni (*folk etymology*)

Mabadiliko ya kileksia pia hutokana na maneno mapya kuibuliwa kutokana na kuumbuliwa au kupindwa kwa maumbo ya yale maneno yaliyomo tayari katika lugha. Mabadiliko yanayofuata mkondo huu hayaongozwi na utaratibu wo wote ule ila tu kupelekea hali ambapo umbo jipya la kileksia litaafikiana na umbo la awali la neno husika.

Etimolojia ya kitamaduni hupelekea ama:

a) Neno kupata fasiri mpya bila ya umbo lake kuathiriwa

au

b) Neno kubadilishwa umbo ili liweze kulingana na elementi nyingine za lugha hiyo.

Hivyo basi, etimololojia ya kitamaduni huathiri tu yale maneno yasiyojulikana kwa urahisi, istilahi za kitaaluma au maneno ya kigeni. Mabadiliko yanayoambatana na etimolojia ya kitamaduni hutokana na hali ambayo kwayo watumia lugha hushindwa kusimilisha maneno hayo ifaavyo katika lugha yao.

2.1.4.3 Ukopaji

Katika lugha yo yote ukopaji ni hali ya kawaida pindi kunapotokea na upungufu wa aina fulani katika mawasilano baina ya watumia lugha. Thomason na Kaufmann (1988) wakinukuliwa na Sankoff (2001) wanaeleza kuwa ukopaji ni ule uingishwaji wa elementi geni katika lugha asili ya mtumia lugha. Myers-Scotton

(1992) anafafanua ukopaji kama ule uingishaji katika lugha maumbo kutoka lugha nyingine. Uingishaji huu unaweza ukajumuisha vipashio vya kileksia au maneno miongoni mwa vipashio vingine vya kiisimu. Ukopaji wa kileksia kwa mujibu wa Massamba (2004) ni “ule ukopaji wa maneno kutoka kutoka lugha chanzo hadi katika lugha lengwa”.

Haugen (1950) anadai kuwa ukopaji ni jaribio la kuzalisha maumbo ya lugha moja katika lugha nyingine. Si lazima lugha inayokopesha iwe na habari kuhusu mchakato huu hali kadhalika si lazima lugha inayokopeshwa itoe kibali.

Hivyo basi, ukopaji ni ile hali ya lugha moja kuchukua maneno au utaratibu wa kiusemaji wa lugha nyingine na kuutumia na hatimaye ukawa sehemu ya lugha hiyo.

Sababu za Ukopaji

Haugen (1950) anadai kuwa ukopaji hutokea katika mazingira ambamo ujozi lugha au ulumbi ni sehemu ya tabia lugha za jamii. Ukopaji vile vile una uhusiano wa karibu na ubadilishaji msimbo. Kwa mujibu wa wataalamu mbali mbali kama vile Sankoff G (2001), Poplack na Sankoff (1984) na Heath (1990) ni ubadilishaji msimbo ambao hupelekea ukopaji. Hata hivyo, tofauti baina ya dhana hizi mbili si ya moja kwa moja. Hii na kwa vile zote mbili hutokea katika mazingira sawia ya wingi lugha.

Kwa mujibu Myers-Scotton (1992), ubadishaji msimbo ni ule uteuzi wa taarifa za kiisimu kutoka lugha moja (lugha bebwa) na kisha kuzihamisha hadi nyingine (lugha solo). Ubadilishaji msimbo hutofautiana na ukopaji kutokana na sababu kuwa yale maumbo yaliyokopwa hatimaye husimilishwa katika lugha ile inayokopa na hivyo kuwa sehemu ya msamiati unaokubalika miongoni mwa watumiaji wa lugha hiyo (Massamba 2004). Kwake Myers-Scotton (1992), yale maumbo ya lugha bebwa hufanywa kuwa sehemu ya umilisi wa kileksia wa mzungumzaji wa lugha solo ukopaji unapotokea. Katika ubadilishaji msimbo, maumbo yaliyohamishwa hutumika

tu kutimizia malengo ya kimkakati ya wakati uliopo. Kutokana na sifa hii, maumbo hayo hayadumu katika lugha.

Akizidi kufafanua kuhusu tofauti zilzopo kati ya ukopaji na ubadilishaji msimbo, Myers- Scotton (1992) anadai kuwa tofauti kati ya ukopaji na ubadilishaji msimbo hujitokeza izingatiwapo kuwa:

- i. Ubadilishaji msimbo ni tukio ambalo huambatana tu na ujozi au wingi lugha miongoni mwa watumia lugha.
- ii. Mtu aweza kujua lugha moja tu lakini akatumia maumbo yaliyokopwa katika usemaji wake.
- iii. Maumbo ya mikopo hujitokeza mara kwa mara katika kopasi sawia na maumbo ya lugha solo. Hali kadhalika, kuwepo kwa maneno ya mkopo katika usemi wa lugha solo kunaweza kutabirika. Kinyume na haya maumbo yanayotokana na uchanganyaji msimbo huenda yasiwe katika kopasi na pia kuwepo kwao si jambo lakutabirika

Maneno ya mkopo huainishwa kwa namna mbali mbali. Kwa mujibu wa Haugen (1950) maneno ya mkopo huweza kuainishwa kama:

- a) Mikopo halisi – kwa maana ya yale maneno ambayo yamekopwa mazima mazima yaani umbo pamoja na maana.
- b) Mikopo iliyohulutishwa (*loan-blends*) ambapo neno la mkopo lina elementi za lugha bebwa kwa upande mmoja na lugha solo kwa upande mwingine jambo linaloibua umbo/neno linalojumuisha sifa za lugha zote mbili.
- c) Mikopo badalia au mikopo ya kisemantiki ambayo ni mkopo inayojumuisha ukopaji wa dhana tu pasipo kukopa neno zima. Mikopo ya aina hii hutokezea kama tafsiri za maana au uigaji wa maana.

Uainishaji huu waweza kulinganishwa na ule wa Yule (1985) ambaye anataja kile anachokiita Massamba (2004) ukopaji sisizi (*calque borrowing*). Anaeleza kuwa ukopaji wa aina hii ni ule unaojumuisha tafsiri ya neno linalokopwa badala ya

ukopaji wa neno lenyewe.

Massamba (2004), anasema kuwa ukopaji sisisi ni “ukopaji wa maana ambapo neno lililokopwa hufasiriwa mofimu kwa mofimu katika lugha inayokopa.”

Uainishaji wa Myers-Scotton (1992) kwa upande wake unatambua aina zifuatazo za maneno ya mkopo:

- a) Mikopo ya kiada (*cultural loans*) ambayo ni maneno yanayoelezea dhana geni katika lugha. Ni maneno ambayo kukopwa kwao ni jambo la dharura kutokana na kuzuka kwa pengo la kileksia litokanalo na lugha kukumbana na hali mpya. Mikopo hii basi hutokea kwa ghafla na hushinikizwa na kuenea kwa matumizi yake miongoni mwa wanajamii walio na ushawishi kubwa
- b) Mikopo ya asili (*core loans*) kwa upande wao ni mikopo ambayo huhusisha maneno ambayo tayari yapo kwenye lugha. Ni zao la uamuzi razini miongoni mwa wanaujozi lugha kupuuza matumizi ya neno ambalo tayari limo kwenye lugha yao na kupendelea neno linalotokana na lugha nyingine. Mikopo hii huanza kama sehemu ya michakato ya ubadilishaji misimbo na hatimaye kutokeza kama maumbo ya kudumu katika lugha.

Myers-Scotton anaendelea kudai kuhusu maneno yaliyokopwa kuwa hutokezea kama:

- a) Sehemu ya umilisi lugha ya makundi fulani katika jamii
- b) Sehemu ya matumizi lugha kimitindo miongoni mwa wanajamii
- c) Jinsi ya kujiimarisha kuihadhi miongoni mwa baadhi ya watumia lugha katika jamii.

Kwa jumla, ukopaji ni njia kuu mojawapo ambayo inapelekea mabadiliko ya kileksia katika lugha. Kinachobainika kutokana na maelezo haya ni kuwa pale ugumu unapotokea katika kufasiri dhana fulani mintarafu ya msamiati uliopo, watumia lugha hubidiwa kukopa kutoka lugha nyinginie wanazozijua. Vile vile ukopaji unaweza

ukashinikizwa na sababu zisizo na umaalum wo wote kiisimu haswa pale ukopaji unapotokea huku kukiwepo na neno mwafaka katika msamiati wa lugha inayohusika.

2.1.4.4 Kubuni Maneno Mapya

Zaidi ya kutokana na ukopaji wa maneno kutoka lugha nyingine, mabadiliko ya kileksia huweza pia kutokana na uundwaji wa maneno mapya kabisa. Kwa mujibu wa Schroeder na D'Arcais (1989), ubunaji huu hutokana na sababu kuwa hakuna lugha yo yote iliyo na maneno ya kutosha kuelezea dhana zote ziwezazo kuzalishwa na watumia lugha. Jambo hili hupelekea kuzuka kwa pengo leksika - yaani ile hali ambapo kunakosekana neno litakaloelezea dhana fulani.

Kutokana na hali hii, watumia lugha hupewa uwezo na lugha kujaza mapengo hayo kwa njia mbali mbali. Tokeo mojawapo ni ubunaji wa maneno mapya. Schroeder na d'Arcais wanadai kuwa kubuni maneno mapya si jambo geni katika lugha (1989). Ni hali inayofaulishwa na weledi wa mazingira ambamo elementi hiyo mpya ilianzishwa na muktadha wa matumizi yake.

Zaidi ya kule kubuni neno jipya kabisa, Yule (1985) anataja njia zifuatazo kuwa zinazotumika pia katika kuunda maneno mapya:

- i. Uunganishaji wa maneno mawili au zaidi ili kuunda neno moja changamani
k.m kiberiti-ngoma
- ii. Uhulutishaji (*blending*) ambapo mwanzo wa neno moja huchukuliwa na kuunganishwa na mwisho au kipande kinginecho cha neno lingine ili kuunda neno moja zima kwamfano-

Chakula cha jioni - chajio

- iii. Uundwaji wa akronimu yaani neno linalotokana na uunganishwaji wa herufi za mwanzo za maneno tofauti katika orodha fulani ili kubuni neno moja fupi kusimamia dhana husika kwamfano –

UKIMWI-. Ukosefu wa Kinga Mwilini

- iv. Udondoshaji ambapo kipashio kimojawapo cha neno huondolewa na hivyo

kupelekea neno fupi lakini lenye maana ile ile kwa mfano:

Boda boda – boda

2.1.4.5 Unururishaji Wa Maana Ya Neno

Mabadiliko pia huweza kutokea kwa kutumia rasilmali iliyopo ya maneno katika lugha yenyewe. Wakati neno linapopanuliwa kimaana na kuwakilisha dhana pana zaidi kuliko lilivyokuwa likiwakilisha awali, mabadiliko husemekana kutokea katika neno hilo kwani limepata dhima mpya katika jukumu lake la kimsingi la kuwa kiashiriaji cha dhana.

Massamba (2004) anataja hali hii kama unururishaji ambao ni “upanuaji wa maana ya neno ili neno hilo liweze kuingiza dhana nyingine zinazokaribiana na ile maana ya awali k.m *kichwa* (cha mwanadamu) lakini pia neno lililo na maana ya kiongozi au sehemu ya mbele ya gari”.

Upanuzi wa maana ya neno hushinikizwa na hali zifuatazo kwa mujibu wa Koch (2002)

- a) Ujirani – iwapo kuna dhana mbili zinazopakana kimaana, neno linaloelezea dhana moja huweza kutumika kuelezea dhana hiyo nyingine ambayo yamkini ni mpya na ina uhusiano wa karibu na ile inayo wakilishwa na neno hilo lililopo.k.m glasi kwa maana ya bilauri yoyote
- b) Mfanano– iwapo dhana mbili tofauti zalingana kwa sifa moja au nyingine, basi jina la moja laweza kutumika kuelezea lingine.
- c) Iwapo kitu huwa sehemu ya kingine, dhana ile iliyo sehemu ya nyingine huweza kuitwa jina moja na ile dhana kubwa.

2.1.4.6 Udondoshaji Wa Maana

Mabadiliko pia huweza kutokea pale fahiwa zinazosimamiwa na neno moja hupunguzwa. Katika hali hii, neno linasemekana kudondosha baadhi ya maana ambazo lilikuwa linasimamia. Hali hii inatokea hasa pale dhana hiyo iliyokuwa ikiwakilishwa na neno hilo inapata neno lingine linaloieleza na hivyo basi kusitisha

matumizi ya hilo neno la kwanza.

2.1.4.7 Utowekaji

Mabadiliko pia huweza kutokea pale matumizi ya neno fulani husitishwa kabisa. Hali hii itatokana na dhana iliyokuwa ikiwakilishwa kutoweka au kubadilika kiasi kuwa neno lile halifai katika kuielezea tena. Katika muktadha wa kazi hii, tunanakili mifano mbali mbali ya maneno ambayo hayatumiki tena kwa kule kupitwa na wakati. Mfano mwema tutakavyoona ni ule wa mfumo wa kuainisha siku za juma na miezi ya mwaka. Katika jamii tuliyoitafiti, matumizi ya mfumo asili wa Ekegusii yametoweka na badala yake maneno mapya yanatumika - maneno yaliyokopwa kutoka lugha za kiswahili na Kiingereza. Mabadiliko ya namna hii yanaakisi hali halisi ya kijamii ilivyo katika mazingira wanamoishi watumia lugha.

Kwa muhtasari basi ni bayana kuwa mabadiliko ya kileksia hujitokeza pale maumbo mapya yanapoingishwa katika lugha. Maumbo haya mapya yaweza kutokea kama maneno yaliyokopwa kutoka lugha nyingine au yaweza kuwa maneno mapya kabisa yaliyoibuliwa kwa njia mbali mbali.

Vinginevyo yaweza kuwa mabadiliko yanayotokea katika kiwango cha kile kinachomaanishwa na neno. Katika hali hii, kipashio cha kileksia huweza kuongezewa maana zaidi au kikapunguziwa maana. Hatimaye, neno lenyewe pamoja na dhana husika huweza kutoweka lisiwe sehemu ya msamiati wa lugha tena.

Yaliyoandikwa Kuhusu Mofolojia

2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mofolojia

Kuna fafanuzi ambazo zimetolewa na wataalamu mbali mbali kuhusu dhana ya mofolojia. Katika kazi hii tuliteua baadhi yazo kwa minajili ya kutupa msingi wa kufafanua dhana ya mofolojia mintarafu ya kazi hii.

Kwa mujibu wa Matthews (1991), mofolojia ni tawi la isimu linaloshugulikia maumbo ya maneno katika miundo na matumizi mbali mbali. Mofolojia kwa ukamilifu wake huchunguza jinsi ambavyo neno linavyoundwa kwa kuainisha vipengele tofauti vinavyolijenga neno hilo. Vijenzi hivi vya neno hutambulika kama

mofimu.

Massamba (2004) katika Kamusi ya Isimu Ya na Falsafa ya Lugha anataja mofolojia kama :

“taaluma ya isimu inayoshughulikia uchambuzi na uchanganuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofimu mbali mbali ili kuunda maneno katika lugha.”

Katika kamusi ya wavuti ya <http://www.thefreedictionary.com> , mofolojia hufafanuliwa kama:

“Taaluma inayotalii muundo na umbo la neno katika lugha kwa kuzingatia vipengele kama vile uambishaji, minyambuliko na uundaji wa maneno changamano”.(TY)

Kwa mujibu wa Mgullu (1999), mofolojia ni:

“Taaluma ya isimu au sarufi ambayo ina jukumu la kuyachunguza maneno ili kuelewa maumbo yake yalivyo.”

Jumla ya yote haya ni kuwa mofolojia huweza kueleza kuwa ile taaluma ya kiisimu ambayo hujishughulisha na jinsi maneno yanavyoundwa. Ni taaluma inayorejelea dhima ya vipashio mbali mbali ambavyo hujenga kipashio cha kileksia. Vipashio hivi vidogo vijulikavyo kama mofimu huelezewa kama vipande vidogo kabisa vya kiisimu vilivyo na uwezo wa kubeba maana..Mpangilio wa mofimu katika neno pamoja na uhusiano baina yazo ndiyo hupelekea neno moja kuwa na faridi na fahiwa mbali mbali. Mofimu zinaweza kuainishwa kama mofimu huru pale zinapojisimamia zenyewe au zinaweza kuwa tegemezi. Mofimu tegemezi hutegemea kuambatanishwa na nyingine ili zikawe na maana. Uhusiano uliopo kati ya mofimu ambazo hujenga neno hujulikana kama uhusiano wa kileksia (Matthews 1991). Uhusiano huu hutawaliwa na kanuni mahsusi za lugha husika.

Utafiti wetu uliangazia michakato mbali mbali ya kimofolojia inayoambatana na vipashio vya kileksia ambavyo vimeathiriwa na mabadiliko kwa minajili ya kueleza jinsi mofimu tofauti hutumika ili kulipa neno jipya uhalisia japo wa kiisimu katika lugha hii.

2.2.1 Uainishaji wa Lugha ya Ekegusii Kimofolojia

Kwa mujibu wa wanaisimu mbali mbali mbali walioitafiti lugha ya Ekegusii, kama vile Whiteley (1960) Cammenga (2002) na Ogechi (2006), lugha ya Ekegusii hutambulika kama miongoni mwa lugha za kilimwengu zinazoegemea matumizi makubwa ya uambishaji katika kuleta maana katika neno. Lugha za aina hii hujulikana kama lugha ambishi- bainishi .Katika lugha za namna hii, viambishi vinapongezwa kabla au baada ya neno athari huzuka sio tu katika faridi ya neno husika bali pia katika fahiwa yake ambayo hubadilika.

Katika lugha ya Ekegusii viambishi huja kabla na baada ya mzizi wa neno. Viambishi hivi huashiria dhana tofauti. Vinapotumika pamoja na mzizi, viambishi hufaulu kuibua neno lenye maana maalum. Msingi wa uambishaji huu huanzia katika nomino na kuathiri aina nyingine za maneno mathalani vivumishi na vitenzi.

Viambishi awali vinavyotumika kuambisha nomina ya Ekegusii vinatokana na mfumo wa ngeli wa lugha ya Ekegusii. Mfumo huu huyaorodhesha majina tofauti katika makundi ya ngeli maalum. Mfumo wenyewe kwa mujibu wa Cammenga (2002) ni kama ufuatao:

Jedwali 1:		Makundi ya Ngeli za Nomino za Ekegusii
Kiambishi		Maelezo
Ngeli		
Umoja	Wingi	
omo	aβa	Majina ya viumbe vyenye uhai, miungu, nafsi
∅	aβa	Majina ya miti, sehemu fulani za mwili, vitu au vifaa mbali
eri	Ama	Vifaa fulani, sehemu za miti, matunda , majina mbali mbali ya
eri	Ama	kawaida Ukubwa usio wa kawaida
eke	eβi	Vitu visivyo hai , vitu vingi vya kila siku, sehemu nyingine za
/eGe		mwili, baadhi ya wanyama , vichaka. Lugha mbali mbali
eke	eβi	Udogo usio wa kawaida
/eGe		

Ke-	Ø	Majina ya sehemu za eneo
e-	či -	Majina ya wanyama wengi , dhana mbali mbali , matukio au vitu mbali mbali
e-n -	či – n-	Majina ya wanyama wengi , dhana mbali mbali , matukio au vitu mbali mbali
aka	eſi	Udogo usio wa kawaida
Oſo -	Ø	Majina ya Kidhahania
ſo-	Ø	Majina ya sehemu mbali mbali za nchi
Okó -	Ama-	Sehemu za viungo vya mwili, nomino za kidhahania za matukio au amali za kijamii
Ko-	Ø	Kitenzi jina
a-	Ø	Mahali / pahali
ŋa	Ø	Majina ya kipekee ya watu, majina maalum ya ng’ombe

Ni viambishi hivi vya ngeli ambavyo vilivishuhudiwa vikijitokeza mwanzoni mwa majina katika lugha ya Ekegusii. Inavyobainika katika maelezo yaliyo katika jedwali hili, hivi viambishi hutekeleza majukumu ya kuyaweka majina katika makundi na kuhakikisha kuwa uanishaji huo kimakundi unaongozwa na taratibu maalum zinazotambulika na watumia lugha.

Hivyo basi, swala la mifanyiko ya kimofolojia liliakisi jinsi ambavyo vipashio vya kileksia vinavyoendelezwa baada ya kupitia michakato ya kimofolojia ya lugha hii.

2.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Lahaja

Wanaisimu hutumia vigezo ainati kupambanua maana hasa ya lahaja. Kwa mfano, katika Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha, Massamba (2004:44) anaeleza lahaja kama:

“Lugha mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kama lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo madogo kama lafudhi au msamiati usio wa msingi.”

Kwa mujibu wa makala ya wavuti ya *wikipedia* ,**Lahaja** ni

“Vilugha vidogovidogo vya lugha moja ambavyo hubainika kijamii au kijiografia. Lahaja za lugha moja zatofautiana katika matamshi, miundo ya sarufi na msamiati.(TY)”

Kulingana na Finnegan na Edward (2007) lahaja ni launi maalum ya lugha inayozungumzwa jamii lugha husika .Katika makala ya *en.wikipedia.org/wiki/Dialect*, launi hii maalum inayotajwa na Finnegan na Edward aghalabu hutambulika kama lahaja badala ya lugha kamili kutokana na sababu kuwa:

- i. Haina mfumo sanifu au uliosimbwa rasmi,
- ii. Haitumiki kwa shughuli zo zote rasmi kama vile katika uandishi na mafunzo,
- iii. Inazingatiwa kuwa ya hadhi ya chini hasa inapolinganishwa na launi zile ambazo zinatambulika kuwa lugha rasmi.

Akichangia Jarida la “*Kiswahili*” 69/2006), Massamba anasema hivi:

“Ili usemaji uweze kuhesabika kuwa lahaja za lugha moja, kuna mambo mawili makuu ambayo hayana budi kuwepo. Kwanza ni lazima sehemu kubwa na ya msingi ya hizo namna mbili za usemaji iwe inachangiwa na namna zote mbili (hasa kimsamiati kimuundo na kimtindo) kiasi cha kuweza kuzifanya kudhihirika kuwa lugha moja. Pili ni lazima pawepo na tofauti za kusemaji baina ya namna hizo mbili kiasi pia cha kuzifanya zibainishwe kama lahaja mbili tofauti za lugha moja. Aghalabu tofauti hizo huwa ni za kimofolojia kimiundo na kimsamiati.”

Kwa mujibu wa Buliba, Njogu na Mwiwaki(2006), lahaja ni vilugha vidogo vidogo vinavyochipuka kutoka kwa lugha moja.. Watu wanaozungumza lahaja fulani hupatikana katika sehemu mahsusi ya kijiografia. Lahaja hizo hutofautiana kwa misingi ya lesksia, kimofolojia, kisintaksia na kifonolojia. Tofauti hizi zinaweza kuwa kubwa au ndogo sana. Lahaja huzuka kutokana na muachano wa kijamii (kitamaduni), kiwakati au kijiografia (kimazingira) baina ya watumia lugha.

Kwa mujibu wa Odeo na Maina (2008) lahaja hutokana na:

“tofauti za kimatamshi na maumbo pamoja na matumizi katika lugha

ambayo huhesabiwa kuwa lugha moja ila hutofautiana katika mambo madogo madogo kama vile msamiati, matamshi, miundo ya maneno, maaana za maneno na sauti.”

Jumla ya yote haya ni kwamba lahaja huchukuliwa kama launi ya lugha moja ambayo ina tofauti ndogo ndogo ambazo zinatokana na misamiati, miundo ya kisarufi na hata matamshi. Tofauti hizi zinatenga launi hii moja kutoka launi inayotumiwa na watumia lugha wengine na hivyo basi kupelekea kwayo kuitwa lahaja. Miongoni mwa mambo yanayochangia kutokea kwa lahaja ni utengano baina ya makundi mawili ya watumia lugha kimasafa au hata kitabaka.

Kufuatana na maelezo haya basi, kuwepo kwa lahaja za lugha ile ile moja ni jambo la kawaida hasa panapo hali ambapo watumia lugha hiyo wametenganishwa na jamii pana ya watumia-lugha wenzao kimazingira au kijamii.

2.4 Hitimisho

Sura hii imeweka wazi mambo anwai yanayohusishwa na mabadiliko ya lugha, dhana za leksia, mofolojia na lahaja kwa mujibu wa wataalamu tofauti. Imedhihirika kuwa mabadiliko hayatokei kiholela bali hufuata mkondo mahsusi kutokana na shinikizo mbali mbali za kiisimu- jamii. Hali kadhalika uchanganuzi wa kazi za hawa wataalamu umedhihirisha kuwa mabadiliko ya kileksia huchukua mielekeo mbali mbali na hatimaye huathiri sio tu mofolojia ya lugha bali pia lugha yenyewe –jambo ambalo linachangia kuibuka kwa lahaja.

SURA YA TATU MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia mbinu mbali mbali zilizotumika katika kukusanya data iliyopelekea kuafikiwa kwa malengo ya utafiti. Uteuzi wa mbinu hizi uliongozwa na sababu kuwa utafiti wenyewe ulikuwa mfano wa utaala wa kilahaja.

Hivyo basi sura hii inazingatia sio tu eneo la utafiti, bali pia watafitiwa na sifa zilizopelekea kuteuliwa kwao kushiriki katika utafiti. Hali kadhalika inaelezea vifaa vilivyotumika kwa utafiti na ufaafu wavyo.

3.1 Eneo La Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika mazingira asili ya kule Goseta. Eneo hili linapatikana kaunti ya Trans Nzoia nchini Kenya. Ni eneo mojawapo kati ya mengine sita katika kaunti hii yaliyo na wingi wa idadi ya wanajamii-lugha ya Abagusii.

Eneo hili lilitolewa hususan kutokana na sababu kuwa linafikika kwa urahisi na pia kwa vile ilichukuliwa kuwa linaakisi sifa bia za maeneo mengine yaliyosakiniwa na idadi kubwa Trans Nzoia.

3.2 Watafitiwa

Kwa mujibu wa takwimu rasmi za serikali, eneo la utafiti la Goseta lilikuwa na wakazi 1289 wakati wa kufanyika utafiti. Hata hivyo ilidhihirika kuwa si wote miongoni mwao walikuwa ni wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii. Kutokana na haya, ilibidi kuwepo na makini katika kuwateua wale ambao wangeshirikishwa kama watafitiwa katika uchunguzi huu.

Baadhi ya vipengele vilivyopelekea kuteuliwa kwa watafitiwa ni pamoja na uwezo wa kuzungumza katika lugha ya Ekegusii, umri wao, kiwango chao cha elimu na iwapo walikuwa walowezi waliotoka kaunti za Kisii na Nyamira au ni vizalia wa

Goseta. Ni wale waliotimiza sifa hizi ambao walijumuishwa katika utafiti.

3.3 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti ulitekelezwa kupitia utumizi wa sampuli mwafaka. Aina mbili za sampuli ziliteuliwa na kutumika kwa pamoja. Aina hizi ni pamoja na sampuli maarubu na pia sampuli nasibu. Sampuli maarubu ilitegemea uamuzi wa mtafiti kuhusu nani hasa angeshiriki katika utafiti huo. Sampuli ya aina hii ilifaa kwa vile aina ya data iliyolengwa ni data yenye upekee na inayopatikana kutoka kwa baadhi ya watafitiwa tu

Umaalumu huu ulikuzwa na sababu kuwa kulitakikana kwa upande mmoja watafitiwa wa umri kati ya miaka 10 hadi 40 kwa minajili ya kuwakilisha vizalia wa Goseta ambao walikulia na kujua lugha sehemu hizo. Kwa upande mwingine kulihitajika watafitiwa wa zaidi ya miaka hamsini. Katika kundi hili kungetarajiwa kupatikana watafitiwa waliokulia sehemu za Gusii na kisha kuhamia Goseta. Ilitegemewa kuwa watafitiwa wa kundi la pili walijifunza na kuijua lugha ya Ekegusii katika mazingira asili kabla hawajahamia eneo la utafiti. Hivyo basi wangetarajiwa kuwa na tajriba tofauti wakilinganishwa na wale watafitiwa wa kundi la kwanza. Isitoshe uteuzi maksudi wa sampuli ungefaa mintarafu ya wakati uliokuwepo wa kufanyia utafiti.

Sampuli nasibu iliteuliwa kutokana na watafitiwa ambao walikuwa wametambulika kuwa walifaa kushiriki utafiti wetu. Sampuli hii nasibu ilipata uamilifu kutokana na sababu kuwa ingekuwa jinsi inayokubalika ya kuondolea mbali uwezekano wa mapendeleo katika utafiti wenyewe. Hali hii ilitokana na sababu ya kuwa uteuzi wa watafitiwa walioshiriki ulikuwa ni wa kinasibu tu na pia kila mmoja kati ya watafitiwa walengwa angetarajiwa kuwa na nafasi sawa ya kushirikishwa katika utafiti huo.

3.4 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ulitekelezwa kwa msaada wa wasaidizi wanne. Wasaidizi hawa walikuwa wawili wa kike na wawili wa kiume ambao waliifahamu lugha ya Ekegusii. Wote walikuwa wakazi wa eneo la utafiti na hivyo basi walitambulika na watafitiwa vyema. Hali hii iliwawezesha kutembelea watafitiwa manyumbani mwao na hata katika sehemu zao za kazi bila kuibua tashwishi miongoni mwao. Isitoshe, wawili kati ya wasaidizi walikuwa wana elimu ya chuo kikuu ilhali wengine wawili walikuwa wamehitimu masomo ya kidato cha nne na kufuzu kwa masomo zaidi. Hali hii iliwafanya kuwa na welewa wa utafiti na malengo yake kwa urahisi zaidi.

Wasaidizi pia walikuwa wa manufaa kwa utafiti huu hasa kupitia mchango wao katika kuyakinisha data iliyokusanywa. Shughuli hii iliendelezwa kwa kuzingatia vipengele mwafaka vya nadharia za usare na vile vile taathira za kijamii. Lengo la kufanya hivi lilikuwa ni kule kuhakikisha kuwa mabadiliko yaliyonakiliwa yalifuata utaratibu mahsusi.

Mbinu na vifaa vifuatavyo vilitumika katika kukusanya data:

a) Uchunguzi wa Nyanjani

Mbinu hii ilitumika ili kubaini moja kwa moja jinsi matumizi ya lugha tafitiwa yanavyoendelezwa katika hali halisi nyanjani. Hali hii iliwezesha utambuzi wa sifa za kileksia zinazojitokeza panapo matumizi ya lugha hii.

b) Matumizi ya Mahojiano ya Ana kwa Ana.

Watafitiwa walihojiwa ana kwa ana na mtafiti au wasaidizi wake ili kupata mwangaza zaidi kuhusu suala la utafiti. Mbinu hii iliufaa utafiti pale palipotukia ugumu katika kuchunguza moja kwa moja jambo fulani au ilipokuwa vigumu kunakili jambo hilo kimaandishi. Mahojiano katika utafiti huu yaliwezesha kupatikana kwa habari kuhusu lugha tafitiwa na tajriba ya watumizi wake.

c) Matumizi ya Hojaji

Hojaji mahsusi iliyotayarishwa kwa ajili ya huu utafiti ilisambazwa miongoni mwa watafitiwa hasa wale ambao wanajua kusoma na kuandika. Ufaafu wa hojaji ulitokana

na sababu kuwa idadi ya watafitiwa ni kubwa na vile vile wamezagaa katika eneo kubwa la kijiografia, jambo ambalo lilihitaji pawepo na mbinu mufti ya kuwafikia watu hawa. Ni kupitia hojaji ambapo habari kuhusu sifa bainifu za matumizi ya lugha katika eneo la utafiti iliweza kupatikana. Habari hizi ndizo zilipelekea uteuzi wa sampuli zilizotumika katika kuufanya uchunguzi kuhusu mada. Hali kadhalika, majibu kutoka hojaji yalizalisha data iliyopelekea maamuzi yanayoangaziwa katika tasnifu hii mathalani habari kuhusu mawanda ya matumizi ya lugha na hadhi ya lugha. Vile vile kwa kuwa muda wa kufanya utafiti ulikuwa mfupi na rasilmali kwa ajili ya utafiti huu kuwa haba, matumizi ya hojaji yalitarajiwa kuokoa muda na pia fedha.

d) Uchanganuzi wa Maandishi Kuhusu Mada.

Utafiti ulijumuisha pia usomaji wa maandishi yote yaliyohusiana na mada katika maktaba na pia kwenye tovuti. Kwa mfano habari sahihi zaidi kuhusu historia ya watafitiwa ilipatikana katika nyaraka za serikali kwenye maktaba za umma na makavazi ya kitaifa. Mbinu hii ya ukusanyaji data ilifaa kutokana na sababu kuwa iliweza kuendelezwa kwa wakati mmoja na mbinu nyingine za ukusanyaji data bila kutatiza ukusanyaji huo. Hali kadhaika, ilidhihirika kama njia nafuu kiwakati na kifedha ya kukusanya data.

3.5 Zana za Utafiti

Zana zifuatazo zilitumika katika kukusanya data nyanjani:

i. Vinasa sauti

Vifaa hivi vilituwezesha kunakili mazungumzo kwa ajili ya kuyafanyia uchanganuzi baadaye na pia kutuwezesha kudumisha hali halisi ya utumiaji lugha kwa kiwango cha kuridhisha. Vifaa vyenyewe vilitumika kurekodia na kuthibithisha kuwepo kwa vipashio vya kileksia ambavyo vilikuwa vigeni. Isitoshe, ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kurejelea habari zilizokusanywa endapo pangetokea tashwishi kuhusu jambo lolote wakati wa utafiti.

ii. Daftari na kalamu

Hivi ni vifaa vilivyokuwa na uamilifu mkuu hasa wakati wa mahojiano kwani

viliwezesha watafiti kufanya unukuzi ipasavyo. Uamilifu wa mbinu hii ulidhihirika pale tulipofanya mahojiano ya mja kwa moja hasa yale yaliyohusu mifanyiko ya kimofolojia. Ilikuwa rahisi kwetu kurudia maumbo ya kileksia tuliyapata pamoja na watafitiwa wetu ili kuhakikisha usahihi wayo.

iv. Diski za kompyuta –

Hizi zimetumika katika ukusanyaji na uhifadhi wa data kutoka tovuti. Vile vile habari zote zilizokusanywa zimenakiliwa na kuhifadhiwa katika vifaa hivi.

3.6 Uchanganuzi wa Data

Kwa vile nyingi ya data iliyokusanywa ilikuwa ni ya kifafanuzi, uchanganuzi wa data ulijihusisha na kuweka pamoja data zote zinazohusiana na kisha kuziainisha kulingana na uamilifu wao kwa malengo ya utafiti. Ni kupitia mbinu za uchanganuzi wa data ambapo tuliweza kutambua vipashio mwafaka vilivyopelekea maamuzi yetu kuhusu mabadiliko ya kileksia na pia kutuwezesha kuratibu mifanyiko ya kimofolojia iliyoambatana na mabadiliko hayo. Matumizi ya majedwali yametumika pia kama mbinu mojawapo ya kuainisha data hasa pale ambapo data hiyo ilihusiana na sifa za kimakundi za watumia lugha. Uchanganuzi huu utabainika zaidi katika sura zifuatazo.

3.7 Hitimisho

Utafiti huu ulikusudiwa kupokea data moja kwa moja kutoka nyanjani ili kuyaidhinisha maamuzi yake. Hivyo basi mbinu na vifaa vilivyotumika viliwezesha watafiti kutagusana na watafitiwa na kupata habari kuhusu mada ya utafiti kwa hali halisi ya nyanjani. Vile vile mbinu zilizotumika ziliwezesha ukadiriaji wa ukubalifu wa mabadiliko na ufaafu wa vipashio vilivyotokana nayo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa na kutumika katika kuandaa sura zifuatazo.

SURA YA NNE
MABADILIKO YA KILEKSIA MINTARAFU YA LUGHA YA EKEGUSII
GOSETA

4.0 Utangulizi

Utafiti huu ulidhukuru na kunakili mabadiliko ya kileksia yaliyoibuka katika launi ya Ekegusii itumikayo katika eneo la Goseta. Katika sura hii, matokeo ya utafiti huo yanawekwa wazi kwa lengo la kuthibithisha kuwa mabadiliko ya kileksia yapo na yamejidhihirisha kupitia mifano mbali mbali ya maneno katika launi ya lugha ya Ekegusii itumikayo Goseta.

Utafiti huu uliibuka na mkusanyikowa mifano anuwai inayoyakinisha kuwepo

kwa mabadiliko ya kileksia katika launi ya Ekegusii itumikayo Goseta. Ni mifano hii ambayo inawasilishwa katika sura hii huku maelezo mwafaka yakitolewa kuhusu taratibu zilizopelekea kutokeza kwayo katika launi hii ya Ekegusii.

Sura hii inadhihirisha aina za maneno yanayoathirika zaidi na mabadiliko na kisha kuyachanganua mabadiliko hayo kwa misingi ya mikabala ya nadharia za usare na taathira za kijamii.

Kulingana na utafiti huu, mabadiliko ya kileksia yalichukua mielekeo mbali mbali ifuatavyo:

4.1 Ukopaji

Ukopaji tulivyotangulia kuona katika sehemu ya 1.7.3 ni ule mchakato wa kiisimu unaopelekea kuingishwa kwa elementi za lugha moja katika lugha nyingine. Katika muktadha wa utafiti huu ukopaji ulijumuisha kule kuingishwa kwa maneno mapya kutoka lugha nyingine katika lugha ya Ekegusii.

Kulingana na uchunguzi huu, ukopaji wa elementi za kileksia uliotokea ulipelekea kuibuka kwa mabadiliko katika launi ya Ekegusii iliyotumika na watifitiwa. Lugha zilizokopesha Ekegusii maneno zilikuwa ni zile za kienyeji kama vile Kibukusu, Kinandi na Kikikuyu na lugha rasmi za taifa za Kiingereza na Kiswahili. Matokeo ya ukopaji yalidhihirishwa kupitia kule kuibuka kwa vipashio vigeni katika launi ya Ekegusii.

Vipashio hivi vigeni vilionekana kufuata mikondo miwili mikuu. Mkondo wa kwanza ulikuwa wa vile vipashio vya kileksia ambavyo vilikuwa na visawe vyao tayari katika lugha ya Ekegusii. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (1992, 2002), mikopo ya namna hii ndiyo hutambulika kama mikopo asili (*core loans*). Mifano tuliyoipata nyanjani ilikuwa kama ifuatayo:

Neno	la Asili	Kisawe	Chake Maana
Mkopo	Yake	Katika Lugha	Ya
1. <i>Omokasa</i>	Kibukusu	Ekegusii <i>Omureti</i>	Mzee wa mitaa

2. <i>Kuka</i>	Kibukusu	<i>Sokoro</i>	Babu
3. <i>Gugu</i>	Kibukusu	<i>Baba</i>	Nyanya
4. <i>Esoteti</i>	Kinandi	<i>Ekerandi</i>	Kibuyu
5. <i>Omorusiki</i>	Kinandi	<i>Amabere Amaroranu</i>	Maziwa mala
6. <i>Ekamuna</i>	Kibukusu	<i>Ekenyamnyonge</i>	Nguchiro
7. <i>Chimbone</i>	Kibukusu	<i>Chinsobosobo</i>	Aina fulani ya matunda
8. <i>Edodo</i>	Kibukusu	<i>Ototo</i>	Aina ya mboga za kienyechi
9. <i>Omosinde</i>	Kubukusu	<i>Omware</i>	Kijana anayejiandaa kupashwa tohara Managu
10. <i>Esucha</i>	Kibukusu	<i>Rinagu</i>	Managu
11. <i>Echebukube</i>	Kibukusu	<i>Eriko</i>	Jiko
12. <i>Echamwaka</i>	Kibukusu	<i>Eguto</i>	Loma
13. <i>Echebira</i>	Kinandi	<i>Ekenyorini</i>	Gunia ya nailoni
14. <i>Emiito</i>	Kibukusu	<i>Enderema</i>	Aina ya mboga za kienyeji
15. <i>Omosiebebe</i>	Kibukusu	<i>Risosa</i>	Matawi ya boga
16. <i>Amabwondi</i>	Kibukusu	<i>Amanyabwari</i>	Viazi vitamu
17. <i>Omkunga</i>	Kiswahili	<i>Omonyenye</i>	Mkunga
18. <i>Omoramwa</i>	Kibukusu	<i>Omoko</i>	Shemeji
19. <i>Chinturantura</i>	Kibukusu	<i>Chintobo</i>	Aina ya mmea wenye natunda madogo makali ya rangi ya mayai (<i>Sodom apple</i>) kwekwe
20. <i>Chikwekwe</i>	Kiswahili	<i>Emetiokia</i>	
21. <i>Okoaro</i>	Kiingerza	<i>Okobosa</i>	Kulima kwa kutumia

			kifaa	maalum
			kinachokokotwa	na
22	<i>Esaiprasi</i>	Kiingereza	<i>Ekerobo</i>	trekta kwa jina haro Aina ya mti
23	<i>Amarura</i>	a Kibukusu	<i>Chinsiaga/</i>	Aina ya nyasi
24	<i>Egeteri</i>	Kikuyu	<i>Amasangaka Chiyoyo</i>	Pure
25	<i>Emesemwa</i>	Kibukusu	<i>Ebirangwati</i>	Zambarau
26	<i>Okara</i>	Kijaluo	<i>Otero</i>	Aina ya viatu
27	<i>Esiango</i>	Kibukusu	<i>Ekenyorini</i>	<i>Kia</i> Kifaa kitumikacho
			<i>Ogwesibia</i>	kujisugua mwili
28	<i>Omoganda</i>	Kibukusu	<i>Ekeombe</i>	unapokoga Kikundi cha
29	<i>Odede</i>	Kibukusu	<i>Egesase/Ribururu</i>	kuchangiana Nzige
30	<i>Mai</i>	Kibukusu	<i>Mama</i>	Mama
31	<i>Chikumbekumb</i>	Kiswahili	<i>Chintuga</i>	Kumbikumbi
	<i>e</i>			
32	<i>Eburugamu</i>	Kiingereza	<i>Omoringamu</i>	mkalitusi
33	<i>Ebakora</i>	a Kiswahili	<i>Enyimbo</i>	<i>Bakora</i>
34	<i>Etreira</i>	Kiingereza	<i>Rigogi</i>	<i>Trela</i>
35	<i>Egamu</i>	a Kiingereza	<i>Oborembo</i>	<i>Gundi</i>
36	<i>Ekaniafu</i>	a Kibukusu	<i>Enyambu</i>	<i>Kinyonga</i>

Inavyobainika hapo juu maneno yaliyokopwa kama mikopo ya asili yametokana na lugha tofauti zinazozungumuzwa na wanajamii lugha walioishi karibu na kutagusana na watafitiwa. Athari za mitagusano hii ndizo zinajidhihirisha katika

vipashio vigeni vya kileksia kama hivi ambavyo tumevinakili hapo juu. Katika muktadha wa utafiti huu, mingi ya mikopo hii ilitokana na lugha ya Kibukusu. Hali hii inaakisi hali halisi ya mambo pale nyanjani kwa vile hii ndiyo lugha ya jamii kubwa zaidi inayoishi Trans Nzoia kulikofanyiwa utafiti. Wanajamii hii pia ndio wanaosakini maeneo mengi yaliyokuwa kwenye ujirani wa eneo letu la utafiti la Goseta.

Mkondo wa pili uliochukuliwa na mikopo uliviweka pamoja vipashio vya kileksia ambavyo havikuwa na visawe dhahiri katika lugha hii ya Ekegusii. Mikopo hii kwa mujibu wa uainishaji wa Myers- Scotton (1992, 2002) ndiyo ijulikanayo kama mikopo ya kiada (*cultural loans*) Mara nyingi ilijumuisha maneno kutoka lugha kama vile za Kiingereza au Kiswahili. Mifano ni kama ifuatayo:

Jedwali 2:

Mifano ya maneno ya mkopo tuliyotagusana nayo ni kama yafuatayo:

Neno La Mkopo	Asili Yake	Maana
<i>Ekayaba</i>	Kiingereza	<i>Aina ya mti wenye miiba unaotumika kuunda ua</i>
<i>Chinyimba</i>	Kibukusu	<i>Nyimbo za tohara</i>
<i>Ewaya</i>	Kiingerez	<i>Waya</i>
<i>Epasi</i>	^a Kiswahili	<i>Pasi</i>
<i>Ekerobu</i>	Kiingereza	<i>Balbu</i>
<i>Eseng'enge</i>	Kiswahili	<i>Seng'enge</i>
<i>Eeka</i>	Kiingereza	<i>Ekari</i>
<i>Esoko</i>	Kiswahili	<i>Soko</i>
<i>Ebucheri</i>	Kiingereza	<i>Kichinjio</i>
<i>Ehavesta</i>	Kiingereza	<i>Mashine malum ya kuvuna nafaka</i>
<i>Estuki/ Esteki</i>	Kiingereza	<i>Mabua ya mahindi yaliyokusanywa pamoja ili</i>
<i>Espreya</i>	Kiingereza	<i>kuyakausha</i> <i>Kifaa maalum cha kunyuyizia kemikali kwa mimea</i>

<i>Embegu</i>	<i>Kiswahili</i>	<i>Mbegu hasa za mahindi</i>
<i>Earo</i>	<i>Kiingereza</i>	<i>Haro</i>
<i>Esabato</i>	<i>Kiingereza</i>	<i>Siku ya kuabudu ya wakristo</i>
<i>Enderi</i>	<i>Kiingereza</i>	<i>Mahali maalum pa kuwakama ng'ombe</i>
<i>Egechinchio</i>	<i>Kiswahili</i>	<i>Kichinjio</i>
<i>Ekabichi</i>	<i>Kiingereza</i>	<i>Kabeji</i>

Ni aina hii ya ukopaji iliyotupelekea kutaka kujua zaidi mambo ambayo yalipelekea kutokea kwake.

4.1.1 Mambo Yaliyopelekea Ukopaji

Ukopaji ulivyojidhihirisha ulionekana kushinikizwa na hali kama vile zifuatazo:

4.1.1.1 Mitagusano

Mojawapo wa visababishi vikuu vya mikopo katika lugha ni mitagusano baina ya wazungumzaji wa lugha tofauti. Katika muktadha wa utafiti huu, mitagusano baina ya Abagusii na wanajamii lugha nyingine zinazosakini maeneo yaliyo katika ujirani wao ulisababisha athari zilizobainika pale kulipoibuka kwa elementi za kileksia za kiajinabia katika launi ya Ekegusii inayotumika Goseta. Mfano tulivyoainisha katika jedwali la kwanza (2.1) ulikuwa ni ule wa vipashio vingi vya kileksia vilivyokopwa kutoka lugha ya Kibukusu kama mikopo asili. Kuwepo kwa vipashio hivi kulitokana na sababu kuwa wanajamii lugha ya wabukusu husakini maeneo mengi yanayozingira eneo la Goseta hivyo kufanya mitagusano ya mara kwa mara lisiloweza kuepukika.

4.1.1.2 Ujozi Lugha

Watafitiwa wengi ilidhihirika walikuwa ni wanaujozi lugha wanawingi lugha. Wengi wao waliweza kuzungumza lugha za Kiswahili na hata Kiingereza kando na lugha ya Ekegusii. Hali hii ilikuwa na athari iliyopelekea kuibuka kwa vipashio vya

kileksia kutoka lugha hizi nyingine katika lugha yao ya mama ya Ekegusii. Kwa mujibu wa Myers-Scotton (2002:239), hii ni kutokana na sababu kuwa mara nyingi wanaujozi lugha huwa na mazoea ya kuchopeka maumbo ya lugha mojawapo kati ya zile wanazozijua katika ile lugha nyingine wanayoizungumza. Hali hii inapokita mizizi hatimaye hupelekea kuibuka kwa elementi ngeni za kileksia katika lugha – jambo linalojitokeza hatimaye kama sehemu ya mabadiliko ya kileksia..

Ni hali kama hii ambayo bila shaka imechangia kule kutokea kwa mikopo kutoka lugha za Kiswahili na Kiingereza tuliyoinakili pale juu katika jedwali la pili.

4.2 Ufupishaji Wa Maelezo Katika Mazungumzo Au Matamshi

Kwa mujibu wa Barber(2006) , mabadiliko huenda yakachochewa wakati mwingine na ile hali ya watumia lugha kupendelea hali yo yote ile inayofanya mazungumzo kuwa rahisi. Mojawapo wa hali hizi ni ile inayodhihirishwa na ufupishaji wa maneno au kupendelea maelezo yo yote yaliyo mafupi hii yamkini ndiyo sababu ya:-

- a. Majina kama vile ya mbolea ya kunyunyizia mimea ambayo wenyeji wataiita “*obwoyo bw’amagoro*” kuitwa “*amonia*” au “*siieni*”
- b. Majina ya miezi ya mwaka ambayo hutajwa kupitia maelezo marefu katika lugha ya Ekegusii k.m:
 - “*omtienyio o’kabere*” au “*monuguno o’barema*” (Februari/mwezi wa pili)
 - “*omtienyio o’kianda*” au “*tureti’akebaki*” (Septemba /mwezi wa tisa)
 - “*omtienyio o’ikomi na kabere*” au “*egesunte kende*” (mwezi wa kumi na mbili/Desemba)

Katika hali hizi, tulipata uwiiano miongoni mwa watafitiwa wa kutumia zaidi utohozi wa maneno ya Kiingereza ya *Februari*, *Septemba* na *Tisemba* au “*Esiguku*” (kutokana na neno la Kiswahili siku kuu) na kwa nadra ile mitajo ya kienyeji.

Katika hali nyingine ilibainika kuwa baadhi ya dhana zinazoelezwa na maneno ya Ekegusii hazina uamilifu wo wote katika mazingira ya Goseta.

Mfano mwema ni ule wa majina ya miti, mimea mbali mbali na wanyama tofauti. Watafitiwa walipotakiwa kutaja miti iliyokuwepo katika mazingira, ni wachache walioweza kuitaja kwa majina ya Ekegusii. Waliposhurutishwa baada ya kupewa vidokezo mwafaka, wengi wao walitumia maneno yaliyokopwa ama kutoka lugha nyingine kama vile ya Kiingereza, Kiswahili au lugha nyinginezo. Sababu kuu ya hali hii ilikuwa ni kwamba miti hii ni ya kigeni isiyojulikana nao katika usuli wa umilisi wao wa lugha.

Mifano

Omokunga badala ya *omonyenye* mti wa Mkunga –

Eburugamu(kutokana na *blue gum*) badala ya *omoringamu*

Embwea (kutokana na neno mbweha) badala ya *ekebwe*

Ekayaba- kutokana na neno la Kiingereza la *kei apple* la mti maarufu utumikao katika kufanya nyua za maboma.

Esuucha badala ya *rinagu* (mboga ya mnavu)

Kamuna (kuchakuro) hamna kisawe katika lugha ya Ekegusii.

Matumizi ya maneno haya yalikuwa yameenea kiasi cha kuwa sehemu ya hata msamiati wa watafitiwa ambao tuliowatarajia kuwa na umilisi zaidi wa lugha hii.

Dhana zingine pia zilionekana kupitwa na wakati. Hali hii hasa inaweza kusemekana kuhusiana na majina ya mwaka yafuatayo ambayo tuliyapata kutoka kwa wazee tu miongoni mwa watafitiwa:

Engatiato – Januari

Monuguno O'barema - Februari

Egetamo - Machi

Rigwata - Aprili

Amaumuntia - Mei

Ebwagi - Juni

Engoromomi - Jiulai

Riete - Agosti

Tureti A'kebaki - Septemba

Esagati - Oktoba

Egesunte - Nopvemba

Egesunte Kende- Disemba

Watafitiwa wa umri mdogo walipotakiwa kuyataja, hamna aliyeweza kufanya vile kwa uhakika. Wale waliojaribu walishindwa kuhusisha jina na mwezi hasa. Hali hii ilionekana pia miongoni mwa hata wazee ambao walionekana kujikanganya kuhusiana na ni mwezi upi unaoitwa jina fulani. Kushindwa kwa watafitiwa kunaeleweka tunapozingatia tofauti za kimazingira baina ya Goseta na Gusii. Mfumo huu wa kuainisha miezi ulikuwa na uamilifu kulingana na misimu ya janibu hizo za Gusii. Hata hivyo, jambo hili lilipochunguzwa kwa kuwatumiwa watafitiwa wa umri mdogo kutoka Gusii, kilichobainika ni kuwa licha ya wao kuujua msamiati huo na hata kuweza kuuhusisha na miezi halisi ya mwaka, ni wachachetu walioweza kukiri kuutumia kuelezea majina ya miezi ya mwaka. Hivyo basi hapakuwa na lingine ila kufikia uamuzi kuwa maneno kama haya yangetumika kama mfano mwema sio tu wa dhana kukosekana katika mazingira bali pia neno kutoweka kutokana na kuwa limekosa uamilifu katika jumla ya tajriba ya mtumia lugha.

Tofauti hizi za kimazingira wakati mwingine pia zilipelekea kukosekana kabisa kwa msamiati mwingine miongoni mwa watafitiwa wazawa wa huku Goseta. Hali hii pia ilidhihirika uchunguzi ulipofanywa kuhusu majina ya matukio mbali mbali ya kimazingira. Kwa mfano kati ya matukio sita yafuatayo, jibu la kuridhisha lilitokea katika mfano mmoja:

- i. Mvua ya vuli - hatukupata jibu
- ii. Mvua ya masika tulipata jibu la “*embura enyinge*”

- ambalo ni tafsiri ya moja kwa moja ya dhana husika
- iii. Kiangazi tulipata jibu la “*omorakera*” ambalo ni sahihi
 - iv. Gharika hatukupata jibu
 - v. Ukungu pia hatukupata jibu
 - vi. Upepo pia hatukupata jibu la kuridhisha

Hali zote hizi ambapo majibu yalikosa zilionekana kutokana na sababu kuwa dhana husika ni ngeni. Kwa mfano, pana msimu mmoja tu wa mvua unaodhihirika katika Kaunti ya Trans Nzoia kinyume na hali ilivyo katika maeneo yanayozunguka Ziwa Viktoria kama vile Gusii ambayo yana misimu miwili mikuu ya mvua kwa mwaka - mvua ya masika na mvua ya vuli. Vile vile, tukio la gharika ni ngeni katika maeneo haya ya Goseta kutokana na sababu kuwa kiasi cha mvua kinachopatikana sehemu hizi ni cha chini ilinganishwapo na Gusii. Ukweli wa kauli hii ulibainika pale tulipopata ya kuwa miongoni mwa wale watafitiwa wazawa wa Gusii hapakuwa na ugumu wo wote katika kutambua dhana zenyewa na kutupa majibu yaliyoafikiana nazo.

Hali sawia na hii ilionekana tulipochunguza maneno yatumikayo katika hesabu. Mara nyingi tulikosa mtafitiwa aliyeweza kuhesabu kupita mia moja kwa kutumia maneno mwafaka badala yake wengi walitumia mfumo wa Kiswahili wa kuhesabu - mfumo ambao bila shaka ni mwepesi ukilinganishwa na ule wa asili.

Mfano:

100 - *emia eyemo* badala ya *rigana erimo*

101 – *emia n’eyemo* badala ya *rigana nang’wanse eyemo*

105 – *emi naisano* badala ya *rigana na ng’wanse isano* n.k

Wengi walishikilia ama kutojua au kuwa huo si mtindo wa kisasa wa kuhesabu. Wale waliojua kwa upande wao walichelea kutumia mtindo huo kwa kuhofia kutoeleweka.

4.3 Mabadiliko Yaliyotokana na Upanuzi wa Maana za Maneno

Katika hali hii, maana za maneno fulani zilipanuliwa ili kuyawezesha kubeba dhana nyingine zenye uhusiano na ile dhana ambayo ilimaanishwa na neno lile awali.

Mifano

“*Omorero*” maana asili ya neno hili ni moto. Katika matumizi yaliyopanuliwa neno hili pia linamaanisha nguvu za umeme

“*Etinga*” kwa maana asili lilimaanisha kile kinu cha kusaga unga. Hata hivyo katika muktadha wa utafiti huu neno hili pia lilimaanisha trekta. Uhusiano ukiwa bila shaka katika ile sifa ya mgurumo utolewao na kinu unaolinganishwa na ule wa trekta. Vile vile trekta sawia na kinu hutoa moshi inapofanya kazi. Kwa hivyo unururishaji ulitokana na mlingano wa sifa

“*Obwoyo*” kwa maana asili humaanisha rutuba au mbolea ya samadi, kwa sasa vile vile ni neno linaloashiria mbolea za kisasa za kemikali zinazotumiwa katika upanzi wa mahindi. Katika mfano huu, unururishaji umetokana na uamilifu wa dhana husika

4.4 Udondoshaji wa Maana

Kulibainika pia na hali ambapo baadhi ya maneno yalipoteza maana zao za awali na badala yake yakatumika kuelezea dhana nyingine mpya.

Mfano

“*Rikorokoro*” ni neno ambalo asili lilimaanisha lori. Hata hivyo katika muktadha wetu, neno hili sasa lilidondosha mofimu [ri-] na kuchukua umbo la [e-] *korokoro* - neno lenye asili ya Kiluhya linalomaanisha mkebe mkubwa utumikao kama kipimo cha mahindi kilicho sawa na uzani wa kilo mbili .

Hali kadhalika, matumizi ya maneno mengine ni muhali katika eneo hili la utafiti. Mfano ni ule wa neno “*richagachaga*” au “*richagara*” ambalo lilionekana kwa nadra sana na badala yake neno “*erori*” kutumika kwa maana ya lori – neno ambalo bila shaka ni la mkopo kutoka Kiingereza na Kiswahili.

4.5 Mabadiliko Ya Kileksia Mintarafu Ya Nadharia.

Kulingana na nadharia ya usare, vibadala vipya havizuki katika lugha kiholela bali hufuata utaratibu maalum. ni huo utaratibu ambao hupelekea vibadala hivi kutambulika kama sehemu ya lugha husika. Kimsingi nadharia hii yadai kuwa vibadala vipya vya kileksia hutokana na hali mbili kuu.

Hali ya kwanza ni ile inayotokea wakati ambapo maneno yanasita kutumika kwa kule kukosa uamilifu katika lugha husika. Hali hii ilibainika pale tulipotaja kutoweka kwa baadhi ya misamiati kwa kupitwa na wakati au kukosa uamilifu katika jamii

Hali ya pili ni ile inaibuka pale ambapo dhana au kitu kipya kinapotokea katika mazingira au pale mazingira yenyewe kwa jumla yanapobadilika. Hii ndiyo hali iliyopelekea kutokea kwa mabadiliko katika launi ya Ekegusii iliyotumika Goseta kwa vile mambo mapya yalionekana kuibukana hivyo kupelekea kuzuka kwa vipashio vipya vya kileksia kupitia ukopaji na utohozi.

Vinginevyo, nadharia hii ya usare yadai kuwa mabadiliko sharti yaongozwe na lengo mahsusi. Ilivyobainika awali (1.6) dhana mpya za kileksia zilijitokeza katika lugha kutokana na kuwepo kwa haja madhubuti, haja hii ilitokea pale ambapo watumia lugha walihisi upungufu katika mawasiliano yao kwa kule kukosa kipashio mwafaka cha kueleza hali iliyowakabili na hivyo kuutatua kwa maneno mapya. Maneno haya yalipoingishwa katika lugha yalitoholewa kiasi cha kuyafanya kuwiiiana na yale ambayo yapo tayari katika lugha. Isitoshe, wananadharia hii wanadai kuwa nia na vibadala pekee havitoshi maadam neno huweza kuingizwa au kukopwa kwa muda mfupi tu kisha likatoweka tena ilivyo na misiimu. Wanasisitiza kuwa sharti neno hili liwe na dhima kamili na wazi katika lugha. Hivyo basi kumaanisha kuwa maumbo ya kileksia hayaingishwi kwenye lugha kiholela. Yale maumbo yanayoibuka yananuiwa kueleza dhana husika na hivyo basi kuafiki maksudi ya mawasiliano vilivyo.

Vingi vya vipashio vya kileksia ambavyo tulikumbana navyo katika utafiti

wetu vilitimiza kanuni hii barabara kwani katika kuviingisha katika lugha, vilitimiza wajibu dhahiri huku kukiwa hakuna vipashio mbadala.

Hta hivyo, licha ya kuwa vipashio vipya vitatimiza kanuni zilizotajwa huwa pana haja ya tathmini zaidi ya vipashio hivyo. Kwa mujibu wa Joseph (1999), watumia lugha mara kwa mara watavihoji yamkini kwa upya wavyo. Kuhoji huku aghalabu hutokea katika kiwango cha kinafisia na kupelekea kubwiwa kwa neno kama sehemu ya msamiati jumla anaoumiliki mtumia lugha. Ni pale mtumia lugha anapotimiza hatua hii ambapo kipashio kipya cha kileksia huwa tayari kuenea miongoni mwa watumia lugha wenzake.

Kwa mujibu wa Anderson (1986:177), kabadala kipya kinapozuka jinsi hii na kukubaliwa na mtumia lugha mmoja, huigwa na wanajamii- lugha husika wengine na kisha huanza kuenea. Hata hivyo, iwapo kutakuwa na kabadala kinza kingine basi vyote viwili hutumika ila baada ya muda, kile kisichopendelewa hutupiliwa mbali.

Swali basi linaloibuka ni lile la vigezo vinavyozingatiwa na hatimaye kupelekea kujikita kwa na kuenea kwa vibadala vipya miongoni mwa watumia- lugha. Hapo ndipo nadharia ya taathira za kijamii inapopata umuhimu wake.

Wananadharia hii huzingatia lugha kama mojawapo wa sifa pambanuzi za utamaduni wa jamii na hivyo basi hupokezwa kati ya wanajamii kama vile sifa pambanuzi nyingine. Kupokezwa huku aghalabu huwa ni kupitia mafunzo na miigo. Hivyo basi wanajamii hujifunza lugha kupitia kufunzwa na kuwaiga wenzao. Kulingana na nadharia, kuzuka na kuenea kwa vipashio vipya katika lugha hutegemea pakubwa ushawishi aliyo nao muasisi wavyo juu ya wanajamii wenzake. Ushawishi huu unatokana na uwezo wake kiuchumi, kisiasa, kijamii, kielimu, kidini, kiumri na kadhalika. Wale wanajamii walio na uwezo huu huweza kuwaathiri wanajamii wenzao kwa urahisi zaidi na hivyo kuwafanya kubadili mienendo yao hadi ikalingana na yao.

Katika utafiti huu ilibainika kuwa wanajamii waliosoma walikuwa na ushawishi jinsi hii. Wao ndio waliibua msamiati mpya katika lugha kutokana na jumla

ya vipashio walivyovipata kupitia elimu yao. Kwa vile elimu mara nyingi iliendelezwa kwa Kiingereza maumbo mengi ya mikopo yaliyoibuka katika utafiti huu yalitokana na lugha hiyo. Hali hii inathibitishwa na sababu kuwa wao walishiriki ubadilishaji msimbo wa urahisi zaidi na pia wakawa ndio waliokopa kwa wepesi. Mikopo hii ndiyo inayojitokeza katika lugha waliyoizungumza na hivyo kuipa sura tunayoipata.

Zaidi ya ushawishi, wananadharia hii pia wanataja ukuruba baina ya wanajamii kuwa hali nyingine inayoathiri kuzuka na kuenea kwa mabadiliko ya kileksia ambayo yalishuhudiwa kwenye utafiti. Ukuruba hupelekea kuzoeana baina ya wahusika jambo ambalo linasababisha kupokewa na kubwiwa kwa maumbo mapya yanayojitokeza katika lugha kuwa jambo rahisi. Hali hii hudhihirika zaidi kundi husika linapokuwa dogo. Wanadai kuwa udogo wa kundi linalopokea mabadiliko huathiri moja kwa moja wepesi wa kuenea kwa mabadiliko hayo. Hali hii ndiyo inayojitokeza katika eneo letu la utafiti na hivyo kuchangia kutokea kwa mabadiliko kwa haraka kwani wakaaji wa Goseta ni wachache na wanaishi kwa pamoja katika eneo dogo jambo linafaulisha ueneaji wa haraka wa vipashio vigeni miongoni mwao.

4.6 Hitimisho

Mabadiliko ya kileksia yaliyotokea basi ni mabadiliko ambayo yamelenga kujaza mapengo dhahiri katika lugha ya Ekegusii yanayotokana na haja ya watumia lugha kujieleza kikamilifu katika mazingira wanamojipata. Inavyodhihirika mengi ya haya mabadiliko yaliathiri nomino – neno linalohusika na kutaja vitu au dhana mbali mbali walizotagusana nazo watafitiwa katika shughuli zao za kila siku. Katika hali zote, mabadiliko yalipotokea yalikubalika na watumia lugha na hivyo basi kuyafanya sehemu ya lugha yao.

SURA YA TANO

MIFANYIKO YA KIMOFOLJIA

5.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia mifanyiko ya kimofoljia ambayo iliambatana na mabadiliko ya kileksia tuliyoyanakili katika sura iliyotangulia. Sura hii, inaweka wazi jinsi ambavyo vipashio vigeni vya kileksia vilishughulikiwa pindi vilipoingishwa katika lugha ya Ekegusii kwa minajili ya kuvifanya kuwiana na vipashio vingine vya kileksia vilivyopo tayari katika lugha yenyewe.

Katika kufanya hivi, utafiti uliangazia misingi ya kimofoljia ya lugha ya Ekegusii ambayo imetumika katika kuainisha mabadiliko ya kimofoljia na kileksia yaliyotokea mintarafu ya launi ya Ekegusii iliyotumika katika eneo la Goseta. Katika kufanya Uchanganuzi vipengee husika vya nadharia za usare na taathira za kijamii vilitumika kwa lengo la kuonyesha jinsi ambavyo elementi mpya katika lugha hushughulikiwa na kuenezwa miongoni mwa watumia lugha. Hatima ya yote haya ni tathmini ya nadharia tete ya utafiti huu kuwa mabadiliko ya kileksia huambatana na

mifanyiko mahsusi ya kimofolojia na hivyo basi kuchangia kuyakuza mabadiliko hayo katika lugha.

5.1 Mofolojia Ya Vipashio Vipya Katika Lugha Ya Ekegusii

Maumbo mapya kileksia tuliyokumbana nayo katika utafiti wetu yalipitia mifanyiko mbali mbali kutegemea na asili yayo. Kwa mfano maumbo yaliyotoka katika lugha ambazo kwazo vipashio vya kileksia huishia konsonanti kama vile Kijaluo au Kinandi yalipitia mchakato maalum ambao ulishuhudia uhawilishaji wayo ili kuyafanya yawiiane na vipashio vyanza katika lugha hii ya Ekegusii. Mchakato huu ulipelekea kuambishwa kwavyo na viambishi tamati vyenye irabu. Kanuni hii ya kuambisha neno na irabu ni kanuni ambayo hushuhudiwa katika lugha zote za Kibantu ikiwemo lugha ya Kiswahili.

Hali hii inadhihirika katika mifano ifuatayo ambapo inabainika kuwa, maneno yote ambayo kawaida huwa yanaishia konsonanti huipoteza yakawa yanaishia vokali:

Neno	Umbo	lililotumika	Neon la Kiswahili
Asili	Nyanjani		
<i>Diesel</i>	<i>Etisoro</i>		<i>Dizeli</i>
<i>Mursik</i>	<i>Omorusiki</i>		<i>Maziwa mala</i>
<i>Nylon</i>	<i>Enaironi</i>		<i>Nailoni</i>
<i>Line</i>	<i>Eraini</i>		<i>Mstari</i>
<i>ruoth</i>	<i>Eruoti</i>		<i>Mfalme</i>

Kanuni hii hata hivyo, haiyaathiri yale maneno yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu kwa vile tayari yalitii kanuni hii.

Mfano:

Neno Asili	Umbo lililotumika	Nyanjani
<i>Chamwaka</i>	<i>Echamwaka</i>	
<i>Lododo</i>	<i>Edodo</i>	
<i>Kamabwond</i>	<i>Amabwondi</i>	

i

Mchakato mwingine tuliounakili ulikuwa ni ule wa kuambisha maneno kwa mofimu mbali mbali. Mofimu zilitokea mwanzoni mwa neno ifwatavyo:

Mfano

Neno	kiswahili	Umoja	Wingi
Diesel	<i>Dizeli</i>	<i>E + Tisoro</i>	$\emptyset + Tisoro$
Suchaa	<i>Mnavu</i>	<i>E+ Suchaa</i>	<i>Chi + Suchaa</i>
Mkunga	<i>Mkunga</i>	<i>O</i>	<i>E</i> +
Chebire	<i>Nailoni</i>	<i>+Mokunga</i> <i>E+Chebire</i>	<i>Mekunga</i> <i>Chi+Chebire</i>
Githeri	<i>Pure</i>	<i>E +Geteri</i>	<i>Ebi+ Teri</i>
Kamuna	<i>kuchakuro</i>	<i>E + Kamuna</i>	<i>Chi</i>
Mulamw	<i>Shemeji</i>	<i>Omo+ramw</i>	<i>+Kamuna</i> <i>Aba</i> +
a		<i>a</i>	<i>Ramwa</i>

Mofimu hizi zilitekeleza majukumu mbali mbali. Jukumu la kwanza ni kuwa zilitekeleza wajibu wa kubeba maana ambayo hatimaye iliathiri fahiwa ya neno lote kwa jumla. Uwezo huu wa mofimu kuathiri maana ya neno unaweza kueleweka vyema zaidi katika usuli wa utaratibu wa uainishaji wa maneno kimofolojia katika lugha ya Ekegusii tuliyouainisha awali. Kwa mfano kiambishi *e-* kinachotangulia maneno kama vile *esuchaa* au *echebira* hutumika kama kiambishi awali cha hali ya umoja ya jina husika. Kiambishi hutumika kwa kuambisha majina yote yanayoelezea dhana au vitu mbali mbali. Hivyo basi kuainisha neno na kiambishi hiki kunachangia katika kuweka wazi fahiwa yake na hivyo kuashiria maana ya neno lenyewe. Hali kadhalika, kiambishi *omo-*(umoja) na *aba*(wingi) hutumika katika kuambisha majina ya vitu vyenye uhai kama vile majina yaelezeayo watu ilivyo katika mfano ambapo neno *omoramwa* humaanisha shemeji.

Vile vile, kule kuyaambisha upya maneno yote yaliyojumuishwa kutoka lugha

nyingine, kulitekeleza jukumu la kuyapa maneno hayo umbo sawia na la majina mengine ya Ekegusii ambayo aghalabu huwa yameambishwa na viambishi awali.

Hali katika kitenzi pia ilionekana kufuatilia ile ya nomino kwani katika kitenzi cha Ekegusii mzizi wa neno hutangulizwa na hata kukamilishwa na viambishi awali na viambishi tamati vyenye majukumu ya kukijenga kimaana kitenzi husika. Viambishi hivi ni kama vile:

- i. Kiambishi cha kiima (hiki hutokana na nomino inayoarifiwa na kitenzi hicho)

Mfano

Omonto (mtu) **O**(kiambishi cha kiima) –*somire* (amesoma)

RI-gori (bei) **RI** (kiambishi cha kiima) –*agure*(imeanguka)

CHI-ng'eni (mboga) **CHI**-(kiambishi cha kiima) – *ayire* (imeiva)

- ii. Kiambishi cha idadi ambacho vile vile hutokana na ngeli husika

Omonto (N) (mtu)	Osomire (T) (amesoma)	Ambapo kiambishi O kinawakilisha mmoja ilhali
Abanto (N) (watu)	BA somire(T) (wamesoma)	BA - kinawakilisha wingi
Eng'ombe(N) (Ng'ombe)	Y Akure(T) (amekufa)	Ambapo kiambishi YA - kinawakilisha mmoja ilhali
Chiombe(N) (Ng'ombe)	CHI akure(T) (wamekufa)	CHI - kinawakilisha wingi
Ekemoni(N) (paka)	GI achire(T) (amekuja)	Ambapo kiambishi GI - kinawakilisha mmoja ilhali

Ebimoni (N) **BIachire(T)** **BI-** kinawakilisha wingi
(Paka) (wamekuja)

iii. Kiambishi cha njeo ambapo kuna kauli tofauti za wakati ambazo huonyeshwa ifuatavyo:

a) Wakati uliopita si muda mrefu:

Kiambishi awali **a** – pamoja na kiambishi tamati –**ete**

Mfano

Kutokana na kitenzi *Beka* (weka) uambishaji huchukua mkondo ufuatao :

A + beka+ ete = **abegete**

b) Jana :

Kiambishi awali **a-**

Mfano

A + beka = **abeka**

c) Asubuhi ya leo :

Kiambishi awali **á** na kiambishi tamati – *ete*

Mfano

Á + beka + ete = **ábegete,**

d) Mapema hivi leo

Kiambishi awali **á**

Mfano

Á + beka = ábeka

e) Wakati uliopita hali endelevu

Kiambishi awali *-ka - (ya)*

Mfano

A + ka+ beka = akabeka

f) Wakati uliopo

Kiamishi tamati *-re (-nre)*

Mfano

- Beka + re = -bekire

Vipashio vya mkopo vilivyonakiliwa nyanjani navyo vilifuatia mfumo huo wa uambishaji :

Kwa mfano, neno *-stuki* lililokopwa kutoka kiingereza kumaanisha kitendo cha kukata mabua ya mihindi na kuyarundika pamoja shambani ili yakauke liliambishua ifuatavyo :

- a) Wakati uliopita si muda mrefu : Kiambishi awali **a** – pamoja na kiambishi tamati **-ete** mfano : **a-situy-eti**
- b) Jana : Kiambishi awali **a-** mfano : **a-situkia**
- c) Asubuhi ya leo :Kiambishi awali **á** na kiambishi tamati – **ete**. Mfano **á –stug-ete**,
- d) Mapema hivi leo :Kiambishi awali **á** Mfano : **á-situkia**
- e) Wakati uliopita hali endelevu :Kiambishi awali **-ka / ya** Mfano (a)- **ya -situkia**,
- f) Wakati uliopo :Kiamishi tamati **-re (-nre)** mfano (o)-**situki-rie**,

5.2 Tathmini Ya Mifanyiko Ya Kimofolojia Katika Lugha Ya Ekegusii

Inavyobainika kutokana na mifano hii, mifanyiko ya kimofolojia iliyotokea haikwenda kinyume na kanuni za kimofolojia za lugha ya Ekegusii. Vipashio vipya vya kieleksia vilichukua muundo wa vile vilivyokuwepo tayari katika lugha. Mathalani nomino zilijumuishwa katika ngeli maalum kwa mujibu wa sifa zao na kuambishwa kulingana na ilivyotakikana katika ngeli hizo. Kwa upande wa vitenzi, michakato ilikuwa ni iyo hiyo kwani kila kitenzi kiliambishwa kwa mujibu wa fahiwa iliyokusudiwa.

5.3 Uchanganuzi Wa Mifanyiko Ya Kimofolojia

5.3.1 Nyanjani

Ilipobainika kuwa neno ngeni linaloingishwa kwenye lugha hufuata mfumo wa kimofolojia wa lugha husika, paliibuka na swala la iwapo palikuwa na uwezekano wa neno lo lote kukubalika kwa misingi tu ya kutosheleza umbo la kimofolojia la lugha. Hali hii ilipelekea uchunguzi zaidi ambapo watafitiwa walipewa mifano ya maneno mbali mbali ya maneno ya kubuni ili kubaini iwapo waliyakubali kuwa sehemu ya lugha yao (*Tazama kiambatisho*). Matokeo yalikuwa yafuatayo :

Swali : Je unakubali kuwa maneno hayo ni ya Ekegusii ?

Jibu:	Ndiyo- 2%
	La – 94%
	Sina hakika – 2%

Kwa mujibu wa Mathews (1991) neno halizalishwi iwapo halitimizi majukumu yoyote katika lugha. Isitoshe, iwapo dhana fulani inawakilishwa na neno lingine katika lugha, hapana haja ya neno jipya. Hivyo basi licha ya kuwa kanuni za uzalishaji maneno katika lugha zinaruhusu maumbo anuai kubuniwa, sio kila umbo linalozalishwa huwa sahihi. Hivyo basi hatukuwa na budi kufikia uamuzi kuwa licha

ya umbo la kileksia kutimiza kanuni zote za kimofolojia mintarafu ya lugha husika, pana vigezo zaidi ambavyo huzingatiwa ili neno likakubalika kuwa sehemu ya lugha hiyo

5.3.2 Kwa Misingi Ya Kinadharia

Hali hii iliwiiana na madai yanayotolewa na Joseph katika ufafanuzi wa nadharia ya usare ambapo anadai kuwa usawa au usahihi wa umbo sio kigezo pekee cha kuidhinisha umbo hilo katika lugha. Sharti kwanza pawepo na sababu madhubuti ya kuingizwa umbo lenyewe katika lugha. Aghalabu sababu hii itatokana na kuwepo na haja ya kuafikia mikakati fulani ya kimawasiliano ambayo haiwezi kutimizwa na maumbo yaliyopo tayari katika lugha hiyo. Hivyo basi haiyumkiniki kuwa maumbo ya kileksia yanaweza kuingizwa kiholela katika lugha. Hii ndio sababu kuu iliyoyafanya mengi ya maumbo tuliyo yawasilisha kwa watafitiwa kukataliwa mbali kwa vile yalikuwa hayana haja kuwepo katika lugha kwa kuwa tayari kulikwa na vibadala vilivyofaa.

Pale ambapo maumbo yalitakiwa, kwa mujibu wa nadharia hii, yalihawilishwa ili yapatane na mfumo bia wa lugha hiyo. Kuhawilishwa huku ndiko kuliwezesha neno kushiriki michakato mingine ya kiisimu katika lugha husika. Hili ndilo jambo lililopelekea maumbo ya kubuni kupita mifanyiko ya kimofolojia kama vile uambishaji ili kuyapa sura na muundo wa maneno ya Ekegusii tulivyoona hapo juu.

Vile vile kulingana na nadharia ya usare, kudumu au kutodumu kwa neno jipya katika lugha kutategemea iwapo neno hilo litaendelea kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa. Kwa hali hii basi, maumbo yanayodhihirisha udhaifu hasa yale yanayorudufisha majukumu ya mengine ambayo tayari yako katika lugha, hayadumu na hutupiliwa mbali pindi kibadala kinachoonekana kuwa kimedumu zaidi kinabainika

5.4 Hitimisho

Mabadiliko ya kileksia katika lugha ya Ekegusii huambatana na mabadiliko ya kimofolojia katika neno husika. Mabadiliko haya ya kimofolojia yanaonekana kuwa na lengo kuu la kuyahalalisha maumbo mageni ya leksia katika lugha.

Hata hivyo, kubadilika umbo pekee sio kigezo tosha cha kuainisha mabadiliko ya lugha kwani lazima pawepo na sababu tosha ya kuthibithisha uhalali wa mabadiliko hayo. Pia, badiliko lo lote lile lawezekana kwa misingi ya kimofolojia lakini katika mkabala wa lugha pana mabadiliko yasiyo halali endapo hayajakubalika na wanajamii.

SURA YA SITA

UCHANGANUZI WA SABABU ZA MABADILIKO YA KILEKSIA MINTARAFU YA LAUNI YA EKEGUSII INAYOTUMIKA GOSETA

6.0 Utangulizi

Pana sababu mbali mbali zinazopelekea kutokea kwa mabadiliko ya kileksia. Katika sura hii ya nne sababu hizi zinachanganuliwa mintarafu ya hali ilivokuwa nyanjani. Sababu hizi zilijumuisha maswala ya kijamii, na kimazingira miongoni mwa sababu nyinginezo.

Ilidhihirika kuwa mabadiliko ya kileksia yalitokana na maswala ya kijamii pale ambapo kuibuka kwa mambo mapya katika jamii kuliakisiwa na mabadiliko katika mfumo wa kileksia wa lugha. Mazingira mapya pia yalitoa mchango wakati dhana ngeni katika mazingira hayo zilidai misamiati mpya - dai lililokidhiwa na kuibuka kwa vipashio vipya vya kileksia. Mabadiliko mengine yanachagizwa na

maswala ya kiisimu pale ambapo kanuni bia za kiisimu -jamii zilishinikiza kutokea kwa maumbo mapya ya kileksia au kugeuka kwa matumizi ya yale yaliyokuwepo.

Katika kuchanganua sababu hizi, utafiti uliegemea pakubwa katika vipengele mahsusi vya nadharia za usare na vile vile nadharia ya taathira za kijamii kuweka misingi ya uchanganuzi . Hivyo basi sura hii inalenga kuchanganua sababu hizi mahsusi za kijamii na kimazingira zilizopelekea kutokea kwa vipashio vipya vya kileksia mintarafu ya launi ya Ekegusii inayotumiwa na wanajamii wa Abagusii wanaoishi kaika eneo la Goseta.

6.1 Sababu Zilizopelekea Mabadiliko Ya Kileksia Kutokea

Kulingana na nadharia za usare na taathira za kijamii, mabadiliko ya lugha na hasa ya kileksia huchagizwa na sababu za kijamii, na za kimazingira. Mabadiliko ya kileksia hutokea pale ambapo elementi zilizopo za kileksia zinakosa uamilifu kutokana na mpito wa wakati na hali katika jamii. Mwelekeo huu wa mambo hupelekea kuibuka kwa vipashio vipya ambavyo vitakidhia mahitaji ya kileksia ya jamii. Kuibuka kwa hivyo vipashio vipya hutokana na mikakati mahsusi ya wanajamii- lugha. Mikakati hii huwezesha na tajriba ya wanajamii - tajriba inayochangiwa na maswala kama vile ya elimu, mitagusano baina ya wanajamii, hali maalum za kimazingira na uhusiano uliopo baina ya watumia lugha .Vile vile kuna swala la uwezo wa baadhi ya wanajamii kushawishi mwelekeo utakaochukuliwa na wanajamii hasa kuhusiana na mabadiliko yanayotokea katika katika lugha yao sababu hizi ndiizo zinachanguniliwa kwa undani zaidi hapa chini :

6.1.1 Elimu

Uchunguzi kuhusu chanzo hasa cha kutokea kwa mabadiliko ya kileksia katika launi ya Ekegusii, ulibainisha elimu kama mojawapo wa visababishi. Ilibainika ya kuwa asilimia kubwa ya watafitiwa waliohojiwa walikuwa wamepata elimu katika viwango mbali mbali. Hali hii inadhihirika katika takwimu zifuatazo zilizozipatikana nyanjani :

Jedwali 2: Tarakimu za Viwango vya Elimu Miongoni mwa Watafitiwa

Kiwango Cha Elimu	Idadi Ya Watafitiwa	Asilimia %
Wasio na Elimu	2	4%
Shule ya msingi	10	24%
Shule ya Upili	22	44%
Chuoni	14	28%
Jumla	50	100%

Tarakimu hizi ziliashiria uwezakano mkubwa wa watafitiwa kuwa na uwezo wa kuzungumza kwa zaidi ya lugha moja. Hii ni kutokana na sababu kuwa elimu ya kisasa katika nyingi ya shule humu nchini huendeshwa katika lugha za Kiingereza na Kiswahili. Katika shule za msingi, lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika madarasa ya kwanza hadi tatu katika sehemu za miji na mashambani kuliko na wanajamii lugha tofauti. Katika viwango vya juu vya elimu Kiingereza ndicho huchukua usukani kama lugha ya mafunzo huku Kiswahili kikitahiniwa kama mojawapo wa masomo yanayofunzwa.

Katika eneo la Goseta, utafiti huu ulibaini ya kuwa hali si tofauti kwani watoto walioenda mashule walifundishwa katika lugha ya Kiingereza na vile vile ya Kiswahili. Hapakuwa na mfano wa mafunzo kutokea katika lugha ya Ekegusii. Hii ilitokana na sababu kuwa shule za umma walizohudhuria watoto wa eneo hili zilihudumia watoto kutoka jamii lugha tofauti. Hivyo basi hali hii ilipelekea kuibuka kwa dhana kuwa mojawapo wa sababu zinazoathiri ukuaji wa lugha ya Ekegusii miongoni mwa wanajamii hawa ni ile sababu kuwa hawana misingi thabiti ya kielimu katika lugha yenyewe. Kwa hakika, katika miaka mingi wanayoelimishwa wanafunzi katika eneo la utafiti hawapewi fursa yo yote ya kujua lugha hii ya Ekegusii kirasmi. Dai hili liliungwa mkono na tarakimu zifuatazo zilizokusanywa nyanjani ambazo zinazodhihirisha kuwa idadi ya wale ambao walidai kupata mafunzo rasmi katika shule ilikuwa ni ndogo ikilingaishwa na ya wale ambao walikosa mafunzo hayo.

Jedwali 3: Idadi Ya Waliojifunza Lugha Hii Rasmi

Jibu	Idadi	Asilimia
Ndio	16	32%
La	34	68%

Wengi wa hawa ambao walidai kuisomea lugha ya Ekegusii shuleni walikuwa wale ambao walizaliwa Gusii kabla ya kugura huko na kuja kulowea Goseta. Hawa walikuwa ni wale watafitiwa wa marika ya juu zaidi miongoni mwa watafitiwa.

Utafiti uligundua kuwa watoto wa Abagusii katika janibu hizi walijifunza lugha ya Ekegusii kutokana na kutagusana na jamaa zao nyumbani na katika mazingira mengine yasiyo rasmi. Kwa mujibu wa Nettle (1990), panapo hali ya kujifunza lugha jinsi hii, uwezekano wa kujifunza maumbo yasiyo sahihi ni mkubwa na matokeo yake hujidhirisha katika mabadiliko ya kileksia. Isitoshe, katika hali ambapo hamna mikakati rasmi ya uwasilishaji lugha, maumbo yasiyo sahihi hujipenyeza katika lugha. Hali hii hupelekea kuibuka kwa launi ya lugha iliyojaa maumbo ambayo hayalingani na yale ya kawaida. Huu ndio mwelekeo ulioshuhudiwa Goseta.

Elimu pia ilionekana kuwa na dhima ya kuathiri mielekeo ya wale waliosoma. Kwa mfano, ni kweli iliyo dhahiri kuwa katika jamii ya kisasa, yule aliyeelimika ana nafasi kubwa zaidi kijamii na kiuchumi kuliko yule asiyeelimika. Kwa mujibu wa Ogechi (2009), mtu kama huyu ndiye huajiriwa kazi na pia kupata fursa nyingi za kujijendesha katika maisha kuliko yule asiyeelimika. Miongoni mwa watafitiwa, hali haikuwa tofauti kwani ilipatikana kuwa wale watafitiwa walioajiriwa na wenye nafasi katika jamii aghalabu walikuwa wamesoma. Matokeo ya hali hii yalikuwa kwamba watu hawa walikuwa radhi kutumia hizo lugha nyingine walizojifunza kama vile Kiingereza na Kiswahili kwa urahisi katika mazungumzo yao na ndio walionekana kuwa na uwezo mkubwa zaidi kuongoza mabadiliko ya kileksia tuliyoyashuhudia kupitia mikopo ya maneno kutoka katika hizo lugha walizojifunza

6.1.2 Ujozi Na Wingi Lugha

Takribani watafitiwa wote ni wanaujozi lugha au wanawingi lugha. Wao huzungumza lugha za Ekegusii na Kiswahili au Kiingereza. Wachache pia walikuwa na ujuzi na umilisi wa lugha nyingine za kienyeji kama vile Kibukusu na Kinandi. Idadi halisi miongoni mwa watafitiwa wetu ilikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali 4: Tarakimu Za Ujozi/Wingi Lugha

Lugha	Idadi Ya Watafitiwa	Asilimi a
Ekegusii, Kiswahili na Kiingereza	37	74%
Ekegusii, Kiswahili na Kiingereza na lugha nyingine za Kiafrika (mf. Kibukusu / Kinandi)	7	14%
Ekegusii na Kiswahili	6	12%

Hali hii inatokana na sababu za kielimu ilivyonekana awali (4.1.1) kwa vile wengi wamepata elimu katika lugha ya Kiingereza. Pia ni hali ambayo imeshinikizwa na sababu kuwa Kiswahili ndicho lingua franca katika janibu hizi. Kule kujua lugha nyingine za Kiafrika kulitokana na mitagusano iliyokuwepo kati ya watafitiwa na wanajamii-lugha husika. Hali hii ya mambo bila shaka ilikuwa na athari dhidi ya lugha ya Ekegusii na ndio sababu iliyopelekea kutokea kwa mifano mingi ya maneno hasa ya Kiswahili na Kiingereza tuliyoyapata katika mfumo wa kileksia wa launi ya Ekegusii iliyotumika na wakazi wa Goseta.

Mwelekeo huu unawiiiana vyema na madai ya wanaisimu kama vile Sankoff na wenzake(2001) wanaodai kuwa panapo na ujozi lugha au wingi lugha, uwezekano wa mabadiliko ya kileksia kutokea huwa mkubwa. Wanaisimu hawa wanadai kuwa wakati wanajamii wanapojifundisha lugha ya pili na kuitumia katika mawasiliano yao ya ila siku, si nadra kupata kuwa vipashio vya kileksia kutoka lugha hiyo ya pili vimevuka mipaka na kujitokeza kama sehemu ya lugha yao ya asili. Mikopo hii

huanza kwa kuwa ya muda mfupi tu lakini baadaye ikadumishwa na kuwa sehemu ya lugha hiyo. Mabadiliko haya ndiyo tuliyoyanakili kupitia mifano ya maneno ya mikopo tuliyoyanukuu katika sura za awali. Hivyo basi ni sahihi kudai kuwa mabadiliko ya kileksia tiliyoyanakili yalichangiwa na kuwepo kwa sifa ya ujozi lugha au wingi lugha miongoni mwa watafitiwa wetu.

6.1.3 Ubadilishaji Msimbo

Ubadilishaji msimbo pia waweza kutajwa kama chanzo kingine cha mabadiliko ya kileksia tuliyoyashuhudia katika utafiti wetu. Ubadilishaji huu kwa mujibu wa Myers- Scotton (1992) huchangia pakubwa katika kufaulisha ukopaji na hivyo waweza kuelezewa kama jiwe la msingi la mabadiliko ya kileksia. Kulingana na matazamo huu wale wanajamii wenye ujozi au wingi lugha hushiriki ubadilishaji msimbo kwa urahisi na hivyo basi kuchangia katika kuingisha vipashio vigeni katika lugha yao. Katika jamii ambayo watu wana viwango tofauti vya elimu, uwezo huu wa kubadilisha msimbo hutegemea kiwango chao cha elimu kwani kuna wale watu waliosoma na wale wasiosoma sana au hata hawajasoma. Hivyo basi, jamii hugawika katika makundi mawili. Kundi la kwanza huwa ni lile la waliosoma. Wale walio katika kundi hili hudhaniwa kuwa na hadhi kuliko wenzao ambao huunda kundi la pili yaani lile la wenye kisomo kidogo na wale wasio na kisomo hata kidogo. Kwa sababu hii, daima lile kundi lisilokuwa na hadhi huwania kuwa kama lile la waliosoma hivyo basi huiga kila kinachotokana na kundi hilo la kwanza. Kuiga huku adai Ogechi (1992) katika tasnifu yake kuanuiwa kuonyesha kuwa wanakundi duni wanahisi kuwa hali yao si ya haki wala halali kwa hivyo wataonyesha kwamba kuwachukulia kuwa wao si wasomi hakufai kwani wao pia wanaweza kusema kwa Kiingereza kama wenzao. Hali hii huwapelekea kuchanganya msimbo. Uchanganyi huu ndio unaozua maumbo mageni katika lugha – maumbo ambayo huweza kuwa ya muda au yakadumu. Maumbo haya yanapodumu hurudi kuwa sehemu ya lugha .Miongoni mwa njia ambazo maumbo hayo hujitokeza huwa ni kupitia vipashio vya kileksia

vilivyokopwa kama vile ambavyo tumevirejelea kwingineko katika tasnifu hii.

6.1.4 Dhima Ya Lugha Ya Ekegusii.

Katika utafiti wetu, tulipata kutambua kuwa lugha ya Ekegusii haikupewa hadhi kubwa na watafitiwa wetu ilivyo na lugha za Kiingereza na Kiswahili. Kwa hakika mawanda ya matumizi ya Ekegusii katika mawasiliano ya watafitiwa wetu hawa yalikuwa finyu mno. Miongoni mwa mawanda ambayo tuliziangatia ni kama vile ya nyumbani, mtaani, kanisani na hata afisini na mazingira mengineo yenye urasmi. Matokeo ya uchunguzi huu yanaelezwa kwa muhtasari kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali 5: Mawanda ya Matumizi ya Ekegusii

Kiwango cha matumizi	MAWANDA							
	Nyumbani		Mitaani		Kanisani		Afisini/Mazingira Yenye Urasmi	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Kila mara	18	36%	8	16%	0	0%	0	0%
Wakati mwingine	28	56%	25	50%	18	36%	14	28%
Kwa nadra	4	8%	17	34%	32	64%	36	72%
Jumla	50	100%	50	100%	50	100%	50	100%

Kutokana na data hii lugha ya Ekegusii ilikuwa na umaarufu zaidi kimatumizi katika mawanda ya nyumbani na mitaani. Katika mawanda ya nyumbani kwa mfano lugha ya Ekegusii ilitumika katika mawasiliano kati ya wazazi na wanao. Vile vile mitaani, lugha hii ilitumika baina ya wanajamii hawa walipotagusana katika shughuli za kawaida za kimaisha. Hata hivyo ni muhimu kuzingatia kuwa umaarufu huu haukuwa wa kiwango cha zaidi ya asilimia hamsini ya watafitiwa. Tulichukulia hali hii kuashiria kuwa lugha hii ilikuwa imeyaachia majukumu yake lugha nyingine – lugha ambazo yamkini ni lugha ya Kiswahili iliyo lingua franca katika janibu hizi au Kiingereza – lugha ya wasomi. Matumizi ya Ekegusii kwenye mazingira yenye urasmi kama vile maabadani na maafisini yalikuwa ya kiwango cha chini. Hali hii imesababishwa na mambo mbali mbali kama vile sababu kuwa mazingira hayo

yamejaa na watu ambao huzungumza lugha tofauti na Ekegusii na hivyo basi kuwalazmu watafiwa tuliowahoji kuweka mikakati tofauti ya lugha ili kuyaafikia malengo yao ya kimawasiliano.

Hali inapokuwa hivi, utumizi wa lugha hupunguka. Kwa mujibu wa Halliday (1978:4 *ktk* Kembo-Sure na Webb) hali ya lugha ni zao la majukumu inayokabidhiwa katika maisha ya watumiaji wake. Hivyo basi lugha kama Ekegusii iliyokabidhiwa majukumu finyu na watumiaji wake inaathirika na mabadiliko kwa urahisi kuliko zile lugha nyingine zinazotumika na wanajamii hawa. Katika kueleza namna athari hizi hutokea kuathiri lugha, Wichman, Stauffer *nw* (2007) wanadahili kuwa lugha isiyotumika sana na wazungumzaji wake ina uwezekano mkubwa zaidi wa kubadilika kuliko ile lugha inayotumika mara kwa mara na wazungumzaji wake. Ni hali kama hii ambayo tuling'amua kuwa ilichangia wepesi wa kuingiliwa kwa lugha ya Ekegusii na maumbo ya kigeni. Jumla ya yote haya ni mabadiliko kwenye vipashio vya kileksia tuliyoyayanakili katika sehemu za awali za tasnifu hii.

6.1.5 Mitagusano

Sababu nyingine ya kutokea kwa mabadiliko ya kileksia ni ile mitagusano baina wanajamii lugha tofauti. Kile kinachotokea ni kuwa elementi za kileksia kutoka lugha hizi tofauti huanza kujidhihirisha katika lugha za wale wanaotagusana. Katika utafiti wetu, tulipata kuwa watafitwa wetu walitagusana sio tuu na Abagusii wenzao bali pia na watu wa jamii-lugha tofauti. Katika mitagusano hii, lugha ya Kiswahili na wakati mwingine pia ya Kiingereza ndizo zilizotumika pakubwa. Hii ndiyo sababu iliyopelekea kutokea kwa mifano mingi ya elementi za kileksia ngeni katika launi ya Ekegusii ilyozungumzwa na watafitiwa wetu.

Ni kuhusu hali kama hii ambapo Aitchison (1996) anadai kuwa, kadiri lugha mbili zo zote zinavyozidi kutagusana kwa kipindi kirefu, ndivyo zinavyozidi kuathiriana. Athari hii hubainika zaidi kupitia katika vipashio vya kileksia. Vipashio hivi adai huathirika kwa vile vina uwezo wa kuenea haraka zaidi baina ya lugha mbili

kuliko vipashio vingine. Kuwepo basi kwa mikopo tulivyoshuhudia kunatokana na hali hii.

6.1.6 Sababu Za Kiuamilifu

Mabadiliko mengi ya kileksia yalionekana kushinikizwa na sababu za uamilifu. Ilibainika kuwa lugha ya Ekegusii mara nyingi ilikosa msamiati wa kuelezea dhana walizokumbana nazo watumia lugha hawa. Kwa sababu hii, walijipata wakikumbana na pengo la kileksia lisiloweza kujazwa kwa njia nyingine ila kwa kukopa kutoka kwa zile lugha walizotagusana nazo zilizokuwa na vipashio mwafaka. Hali kama hii ilidhihirika kwenye duka la kuuza vifaa vya nguvu za umeme katika eneo hili ambapo muuza duka Bw. Richard Mochere hakujua iwapo kulikuwa na msamiati wote wa Ekegusii unaoeleza vifaa vya nguvu za umeme tulivyo vipata pale dukani ndiposa tukawa na maneno kama yafuatayo:

Ekerobu(tunguu/glopu)

Epaipu(mwanzi)

Esoketi(soketi)

Emita(mita)

Katika mfano kama huu, dhana hizi za kigeni zilionekana kuelezewa vizuri zaidi na maneno haya yaliyokopwa kwa vile lugha ya Ekegusii haina maneno mbadala yanayoweza kutekeleza jukumu hilo. Mabadiliko ya aina hii yanaonekana kuelekezwa na kupanuka kwa matumizi yanayodaiwa lugha na hivyo basi kutokea kwayo ni jambo la kutarajika katika hali kama hi ambapo hamna vidadala mwafaka katika lugha ya Ekegusii. Kwa mujibu wa Crowley (2000), upeo wa matumizi ya lugha unapopanuka, baadhi ya vipengele vya lugha hiyo hulazimika kubadilika ili kukidhia hali hii mpya. Kipengele mojawapo ambacho huathirika kwa urahisi ni kile cha kileksia ambacho hushuhudia mabadiliko yanayojumuisha uingizwaji wa vipashio vipya katika lugha ili kuelezea dhana mpya zinazozuka katika tajriba ya watumia –lugha.

6.1.7 Sababu Za Kimazingira

Mabadiliko yalitokana na tofauti dhahiri zilizopo kati ya mazingira ya Gusii kulikochipukia lugha ya Ekegusii na maeneo ya Trans Nzoia wanakoishi watafitiwa wetu. Hali hii ilijidhihirisha pale tulipowapa watafitiwa orodha yenye maneno ya Ekegusii. Wengi wao walishindwa kuzitambua yamkini kwa vile yale yanaoelezewa na maneno hayo ni dhana ambazo hupatikana janibu za Gusii. Hata hivyo, wale watafitiwa wazee ambao ni wazaliwa wa Gusii walizitambua mara moja. Mathalani majina ya mwezi yana msamiati mwafaka katika lugha ya Ekegusii. Majina aya hata hivyo hayajulikani miongoni mwa watafitiwa wengi wazaliwa wa Goseta. Hii inatokana na sababu kuwa mara nyingi yakibuniwa na kutumika yalikuwa na maana mahsusii iliyolingana na matukio ya kimazingira yaliyokuwa yameshamiri kule Gusii na ambayo hayapo Trans Nzoia. Mfano mmoja dhahiri ni kuwa kule Gusii ivyoelezwa na baadhi ya watafitiwa, misimu ya upanzi huwa ni miwili katika kipindi cha mwaka mmoja ilhali Goseta na maeneo ya Trans Nzoia, msimu ni mmoja. Isitoshe nyakati kama vile za kiangazi hutokea kwa wakati tofauti katika maeneo yote mawili. Matukio haya ndiyo huwa msingi wa msamiati ya Ekegusii inayoelezea miezi ya mwaka. Hali kadhalika, matukio Fulani ya kimazingira yanayotokea Gusii hayashuhudiwi Trans Nzoia. Mfano mwema ni ule wa zile pepo zinazovuma kutoka Ziwa Viktoria hadi vilima vya Gusii nyakati fulani za mwaka. Pepo hizi zina msamiati wake maalum ambao haukufahamika miongoni mwa watafitiwa kwa vile hauna maana yo yote kwao. Ni tofauti kama hizi na nyingine nyingi za kimazingira ambazo zinachangia hali ambapo msamiati fulani unatoweka na mwingine hata kuchukua maana tofauti na ilivyo kusudiwa na watumia lugha.

6.1.8 Shughuli Za Kilimo

Shughuli kuu ya kiuchumi Goseta ilivyo na kule Gusii ni kilimo. Tofauti hata hivyo huzuka pale tunapozingatia kuwa katika janibu za Goseta kilimo

kinachoendelezwa ni kile cha kisasa. Kilimo hiki kinajumuisha ufugaji wa ng'ombe wa gredi, na upanzi wa mimea kwa ajili ya kujipa mapato. Tofauti hizi ndizo zilionekana kupelekea kuibuka kwa upekee wa msamiati unaoambatana na shughuli hizo za zaraa. Mathalani katika ukulima wa mahindi ambao ndiyo shughuli kuu ya wakaazi wa Goseta, paliibuka na misamiati inayoelezea utumizi wa mbegu maalum za mahindi, unyunyizaji madawa ya kuuu magugu na wadudu waharibifu na hata uandalizi wa mashamba na uvunaji wa mahindi yenyewe. Hali kadhalika katika ufugaji wa ng'ombe, misamiati mipa iliibuka ambayo huelezea mifugo wanaofugwa na waakaaji wa Goseta. Matokoeo ya haya yote yalikuwa misamiati kama vile:

Neno	Maana
<i>Embegu</i>	kutokana na neno mbegu kumaanisha mbegu maalum ya mahindi inayopandwa na wakulima wa zao la mahindi
<i>Emborea</i>	kutokana na neno mbolea kwa maana ya mbolea ya kenikali inayotumika kurutubisha mashamba
<i>Espreii</i>	kutokana na neno spray kwa maana ya kemikali zinazonyunyiziwa mashamba kuuu wadudu na magugu
<i>Chikwekw</i>	kutokana na neno kwekwe kwa maana ya magugu
<i>e</i>	
<i>Chiteresi-</i>	kwa maana ya <i>terraces</i> – mitaro maalum inayotenganisha mashamba kwa minajili ya kuzuia mmonyoko wa udongo
<i>Chistuki</i>	kwa maana ya <i>stooks</i> kusanyiko la mahindi makavu shambani
<i>Amasakari</i>	kwa maana ya majani makavu ya mahindi shambani
<i>Efresiani-</i>	kwa maana ya <i>Friesian</i> aina ya ng'ombe wa gredi
<i>Egansi</i>	kwa maana ya <i>Guernsey</i> aina ya ng'ombe wa gredi
<i>Echasi</i>	kwa maana ya <i>Jersey</i> aina ya ng'ombe wa gredi

Tofauti nyingine ilijitokeza kwa vifaa vya kilimo. Tulipata kuwa vifaa vya kisasa vya kilimo ndivyo vilitumika kufanya kazi za shambani. Kwa vile vifaa hivi ni

vya kigeni havikuwa na majina mwafaka katika lugha ya Ekegusii – jambo ambalo lilipelekea kuibuka kwa maneno mapya kuelezea dhana husika kama vile:

Neno	Maana
<i>Ekeragit</i>	kwa maana ya trekta
<i>a</i>	
<i>Earo</i>	kwa maana ya kifaa maalum cha kulima shamba kiitwacho <i>harrow</i> kwa Kiingereza
<i>Epranta</i>	kwa maana ya <i>planter</i> kwa Kiingereza -mtambo unaotumika kwa ajili ya upanzi wa mahindi na ngano
<i>Etira</i>	kwa maana ya <i>tiller</i> kwa Kiingereza – mtambo maalum unaotumika kuchimba mitaro ya kupandia mahindi
<i>Ehavesta</i>	–kwa maana ya <i>harvester</i> kwa Kiingereza – mtambo maalum unaotumika kuvunia mahindi au ngano shambani

Sambamba na kuibuka kwa majina mapya, palinakiliwa pia na mifano ya utowekaji wa msamiati asili wa Ekegusii ambao ulitumika kelezea baadhi ya dhana. Mfano mwema hapa ni ule wa majina ya ng’ombe waliofugwa. Msamiati uliotumika kutajia ng’ombe waliofugwa na Abagusii zamani ambao aghalabu walikuwa wa kienyeji ulitegemea kuwapa ng’ombe majina kwa misingi ya rangi zao kwa mfano:

<i>Nyang’era</i>	Ng’ombe mweusi
<i>Nyandabu</i>	Ng’ombe mweupe
<i>Nyaibu</i>	Ng’ombe wa rangi ya kijivu

Jumla ya yote ni kuwa misamiati mipya ilizuliwa na mabadiliko katika shughuli za kiuchumi za wanajamii. Mengine nayo ilitoweka kwa kukosa uamilifu katika mazingira mapya ya watumia lugha hawa.

6.1.9 Sababu za Kiisimu

Katika uchanganuzi wetu wa mabadiliko ya kileksia tulikabiliana na hali ambapo misamiati ya lugha tafitiwa ilitoweka isijulikane miongoni mwa watafitiwa huku sababu kuu ikiwa ni kuwa ilikosa uamilifu katika maisha ya watumia lugha. Vinginevyo, tulishuhudia kupanuliwa kimaana kwa baadhi ya misamiati. Hali hii iliposhuhudiwa kulikuwa na ukuruba wa kimaana kati ya dhana iliyowakilishwa awali na neno husika na ile inayojumuishwa katika hali hiyo mpya. Mifano ya hali hii ni ile tuliyoinkuu (uk 63) ya:

omoro ambao kwa asili humaanisha moto lakini pia sasa humaanisha nguvu za umeme

Etinga kwa maana asili lilimaanisha kile kinu cha kusaga unga na hivi sasa hutumika kwa maana ya trekta.

Obwoyo kwa maana asili humaanisha rutuba au mbolea ya samadi, kwa sasa vile vile ni neno linaloashiria mbolea za kisasa za kemikali zinazotumiwa katika upanzi wa mahindi.

Hali hii inaelezewa na wataalamu kama vile Halliday (1978) na Crowley (2000) ambao wanadai kuwa jinsi lugha ilivyo ni zao la majukumu ambayo imepangiwa kutekeleza katika maisha ya watumiaji wake. Kutokana na dai hili ni dhahiri kuwa mabadiliko katika mahitaji na matarajio ya wanajamii kwa lugha yao yakibadilika, basi lugha haina budi kubadilika pia. Kwa upande wake mikakati ya namna hii ndiyo huunda msingi wa mabadiliko ya kianalofia pale ambapo dhana zinaonekana kupewa majina kutokana na uhusiano wa kisifa uliopo baina yazo.

6.1.10 Idadi Ya Watumiaji Lugha

Ilivyodokezwa hapo awali (uk 43), eneo la Goseta lina jumla ya wakaaji 1289- idadi hii ikiwa ni ya watu wazima pamoja na watoto. Katika kundi la udogo huu, yawezekana kwa jambo jipya kama msamiati mpya kuenea kwa kasi na kwa wepesi kwa vile watumia lugha husika wanaishi pamoja na kushiriki hali sawa za kimaisha

na kimazingira kila siku . Hivyo basi changamoto zinazowakabili kwa sehemu kubwa hulingana na hivyo huwashinikiza kukumbana nazo kwa njia maalum zilizo dhahiri na ambazo huigwa kwa haraka baina yao. Matokeo ya yote haya ni vipashio mbadala vya kileksia tulivyovinakili.

Dai hili linapata uungwaji mkono katika tafiti zilizofanyika kwingineko na wanaisimu mbali mbali kama vile Nettle (1999b *katika makala ya wavuti ya www.staff.ncl.ac.uk/daniel.nettle/lingual.pdf*) ambaye anadahili kuwa kadiri kundi la watumia lugha linavyokuwa ndogo ndivyo nayo mabadiliko yanavyotokea nakeuenea kwa urahisi. Wichmann, Staufer na wenzao (2007) pia wanathibithisha madai haya wakitumia mjarabati wa taraklishi na kuongeza kuwa kundi kubwa la watumia lugha huchukua muda mrefu kuyapokea na kuyakubali mabadiliko ya lugha kuliko kundi dogo.

6.1.11 Utengano

Uchunguzi wetu ulibaini kuwepo kwa mwachano baina ya wazungumza lugha ambao ulikuwa na athari kubwa dhidi ya lugha yenyewe. Mwachano huu ulikuwa katika ngazi mbili. Kwanza kabisa ulikuwa ule utengano kati ya vizazi vya awali na vile vya kisasa katika jamii hii. Ilibainika kuwa wazee wengi hawakuwa wamesoma kama wanao na vijukuu wao hivyo basi kupelekea kuibuka kwa tofauti za kimtazamo kuhusu maisha na maswala mengineo ya kijamii. Mwachano huu uliidhihirika katika muktadha wa utafiti wetu pale ilipobainika kuwa ulikuwa na athari dhidi ya uwasilishaji lugha baina ya vizazi. Kwa hakika, wazee wengi walilalama kuhusu kukosa nafasi ya kutagusana na wanao na hata wajukuu wao na hivyo basi kukosa fursa ya kuwasaidia katika kukuza na kuendeleza lugha ya Ekegusii katika jamii hii. Hali hii ilitoa nafasi kwa vipashio vigeni vya kileksia kujipenyeza na kukita mizizi katika lugha ya Ekegusii inavyobainika katika mifano ifuatayo ya mazungumzo baina ya mtafiti na watafitiwa wawili wenye umri tofauti:

Pili, tulitambua pia kuwa lugha ilibadilika kutokana na utengano wa kimasafa

kati ya watafitiwa wetu na jamii pana ya Abagusii huko Gusii. Umbali kati ya Gusii na Goseta ni wa zaidi ya kilometa mia tatu na hugharimu kiasi kikubwa cha nauli. Hivyo basi mitagusano baina ya watafitiwa hukabiliwa na vizuizi ambavyo hukuzwa mwachano huu na kupelekea mitagusano michache tulivyobaini katika utafiti wetu. Ilibainika kuwa endapo watafitiwa wangepanga safari kwenda Gusii, walienda kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maswala ya dharura kama kuhudhuria mazishi au arusi. Kwa hali hii basi ilikuwa vigumu kwao kudumisha hali sambamba ya lugha baina yao na aila zao kule Gusii. Hali hii ilikuwa na uzito zaidi miongoni mwa watafitiwa vijana ambao walikuwa na mitagusano michache zaidi ikilinganishwa na ya wale watafitiwa wa umri mkubwa.

6.2 Hitimisho

Sura hii imejikita katika kutalii na kupembua sababu mbali mbali zilizopelekea mabadiliko ya kileksia kutokea katika launi ya lugha ya Ekegusii iliyotumika Goseta.

Ilivyodhihirika, mabadiliko ya kileksia yanapotokea huakisi mambo yalivyo katika jamii kwa mujibu wa hali za kijamii, kiuchumi na kitamaduni. Panapo mabadiliko katika hali hizi, lugha hubadilika ili kutimiza mahitaji ya wanajamii katika kuwasilisha hali yao hiyo. Mojawapo wa vipengele vinavyoathirika kwa wepesi ni kile cha kileksia kwa vile vipashio vya kileksia ndivyo huwa katika mstari wa mbele katika kuelezea hali hizo ngeni. Kuhusu hali hii, Aitchison (1996: 116) anadai kuwa ni rahisi kwa vipashio hivi vya kileksia kuingizwa katika lugha kwa vile havina athari kubwa kwa muundo wa lugha ambayo huvipokea.

Vile vile, katika utafiti huu, tuling'amua kwa mfano kuwa kusambaratika kwa mifumo asili ya kijamii kulikuwa na athari dhidi ya uwasilishaji lugha – jambo ambalo lilirahisisha ujipenyezaji wa maumbo mageni katika lugha hata wakati kulikuwa na vidadala mwafaka.

Jumla ya yote haya hata hivyo ni kuwa mabadiliko yanapotokea katika lugha

hayatokei kiholela bali husababishwa na sababu dhahiri katika jamii na katika mazingira ambamo lugha hiyo hutumika kwa lengo moja kuu ambalo ni lile la kuyakidhia mahitaji mahsusi ya kimawasiliano ya wanajamii –lugha husika.

SURA YA SABA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

7.0 Hitimisho

Utafiti huu ulikusudiwa kudhukuru mabadiliko ya kileksia na michakato ambatani ya kimofolojia ambayo ilijitokeza katika launi ya lugha ya Ekegusii inayotumika na wanajamii lugha wa Abagusii wanaoishi katika eneo la Goseta wilayani Kwanza katika kaunti ya Trans Nzoia.

Kupitia ukusanyaji na uchanganuzi wa data kutoka nyanjani, na pia utafiti wa maktabani, tuliweza kubaini kuwa launi hii ilikuwa inasheheni mabadiliko mengi na ya aina mbalimbali ya kileksia. Mabadiliko haya yalitokana na utowekaji wa msamiati asili kutoka kwa lugha, kupanuka kimaana kwa mingine huku mingine mipya ikiongezwa lughani kupitia mbinu ya ukopaji.

Mabadiliko haya yote yalichunguzwa chini ya mkabala wa nadharia za usare na taathira za kijamii ambazo zilipelekea welewa wa michakato inayoibua mabadiliko ya jinsi hii katika lugha.

Isitoshe, tulidhihirisha mifanyiko ya kimofolojia inayoambatana na mabadiliko haya hivyo kutupa ufahamu wa zile kanuni zinazozingatiwa pale maumbo mbadala tuliyoyanakili yanapodhihirika katika lugha.

Utafiti pia ulipata kuunga mkono madai ya wanaisimu kuwa katika lugha yo yote ile inayopitia mabadiliko pana vipengele ambavyo hubakia imara kwa kipindi kirefu huku vingine vikibadilika kwa wepesi zaidi. Hali hii ilidhihirika pale tulipong'amua kuwa kati ya vipengele tulivyo vitafitia katika lugha ya Ekegusii, ni

kipengele cha leksia kilichoathirika zaidi na kwa wepesi huku kile cha mofolojia kikibakia thabiti.

Data tuliyoipata kutokana na utafiti huu vile vile ilituwezesha kudahili kuwa launi tuliyoifanyia utafiti yaweza kutajwa kama mfano wa lahaja inayoibuka ya lugha ya Ekegusii. Uamuzi huu ulifikiwa kwa kuzingatia vipengele ambavyo vimetumika kwingineko katika kuainisha lahaja za lugha na hasa lugha ya Ekegusii na watafitiwa tofauti katika nyakati mbali mbali.

Mojawapo kati ya vigezo vinavyotumika katika kutaja launi yo yote ile kama lahaja ni kile kigezo cha muachano wa kimasafa na wakati baina ya makundi ya watumia lugha. Hali hii tulivyoona katika utafiti huu imeathiri watumia lugha hii ya Ekegusii walioishi Goseta. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa maumbo anwai ya kileksia ambayo hayalingani na yale ya lugha asili ya Ekegusii. Kutokea kwa maumbo haya kulionekana kutokana na sababu hii ya muachano wa kiwakati na kitalifa baina ya Gusii na Goseta. Jambo hili la pili haswa lilikuwa na athari kubwa zaidi dhidi ya lugha inapozingatiwa kuwa umbali baina ya maeneo haya mawili ulichangia kuwepo na mitagusano ya nadra baina ya watafitiwa na aila zao huko Gusii.

Kimazingira pia mandhari ya Goseta na yale ya Gusii ni tofauti hivi kwamba dhana zinazopatikana huku Goseta ni tofauti na zile zilizo Gusii hivyo basi kupelekea kutokea kwa msamiati mpya - msamiati ambao waweza kutumika kama kigezo cha uainishaji wa lahaja kwa misingi ya maelezo ya lahaja tuliyoyanukuu pale juu.

Isitoshe, kuna mwachano wa kijamii baina ya watafitiwa hivi kwamba vizazi vya awali na vya sasa vina mielekeo tofauti kuhusu mambo mengi ya kimaisha kukiwemo lugha. Tumbaini ya kuwa mitagusano baina ya wazazi na wanao au wajukuu wao ni michache kutokana na tofauti zinazotokana na maswala kama vile shughuli za kila siku wanazozishiriki watafitiwa. Kwa mfano watoto hutumia wakati wao mwingi wakiwa shuleni au wakicheza huku wazazi wakiwa makazini wakitafuta

riziki. Jambo hili tulivyotangulia kutaja liliathiri jinsi lugha inavyowasilishwa na kukuzwa miongoni mwa wanajamii na hivyo basi kuchangia kuzuka kwa mabadiliko. Ni mabadiliko haya ambayo yanaweka msingi wa kuibuka kwa tofauti katika lugha zinazochangia madai kuhusu uwezekano wa kuibuka kwa lahaja ya Ekegusii miongoni mwa watafitiwa.

Kigezo kingine kilichotumiwa na wataalamu mbali mbali kuainisha lahaja ni ile hali ambapo lahaja huzingatiwa kuwa mfano duni wa lugha kuu. Tulivyoona katika sura tangulizi, wanajamii hii aghalabu huitumia lugha ya Ekegusii katika shughuli zisizo na hadhi au urasmi kama vile mawasiliano ya nyumbani na mitaani. Vile vile, wengi walihisi kuwa Ekegusii kinachozungumzwa baina yao ni cha kiwango duni ikilinganishwa na cha wenzao waliozaliwa Gusii kabla ya kugura hadi maeneo ya Goseta. Hivyo basi huu mwelekeo hasi kuhusu lugha waliyoitumia wakaaji wa Goseta wawezakuchukuliwa kama kigezo kingine cha kuainisha launi yao ya Ekegusii kama lahaja.

Hali kadhalika data tuliyoipata ilidhihirisha kuwa watafitiwa wengi waliozaliwa katika eneo la utafiti walikuwa na umilisi wa lugha tatu jambo lililoathiri pakubwa uteuzi wa vipashio vilivyotumka katika mawasiliano yao na hatimaye kuchangia kubwiwa kwa baadhi yavyo kama sehemu ya lugha ya Ekegusii. Hali hii ni sawa na ile anayoianisha Cammenga (2002) pale anapotambulisha lahaja ya mijini kule Gusii kwa misingi ya kuwa imeibuka miongoni mwa watumia lugha wenye sifa ii hii ya wingi lugha.

Mitagusano na wanajamii- lugha tofauti ni kigezo kingine kilichotajwa kuwa sababu ya kuibuka kwa lahaja kinachojitokeza katika muktadha wa utafiti wetu. Tunaporejelea uainishaji wa Whiteley(1960) na Ogechi(2006), msingi wa utambuzi wa lahaja za Ekegusii za *Rogoro* na *Maate*, ni vipashio vya kileksia ambavyo vina asili ya lugha za Dholuo na Kikipisigis. Vipashio hivyo vinadaiwa kuwa zao la mitagusano baina ya jamii ya Abagusii na majirani zao Wajaluo.

Mfano wa vipashio hivi ni kama vifuatavyo:

Maate	Asili	Rogoro	Maana
	(Dholuo)		
<i>Ebeti</i>	<i>Bet</i>	<i>Omoro</i>	Upanga
<i>Amarabuoni</i>	<i>Rabuon</i>	<i>Amanyabwar</i>	Viazi Vitamu
		<i>i</i>	
<i>Ebiduma</i>	<i>Oduma</i>	<i>Chibando</i>	Mahindi
<i>Egutwa</i>	<i>Ogudu</i>	<i>Ekobia</i>	Kofia
<i>Egoti</i>	<i>Got</i>	<i>Egetunwa</i>	Kilima
<i>Ekerundu</i>	<i>Orundu</i>	<i>Egeticha</i>	Kishamba

Ni uainishaji huu unaotuelekeza kudahili kuwa launi ya Ekegusii inayotumika na wakaaji wa Goseta ni mfano wa lahaja ibuka kwa vile watafitiwa wetu kama vile wenzao wa Gusii wamekuwa na mitagusano na wanajamii-lugha nyingine. Jambo hili lilipelekea kuibuka kwa maumbo ya kileksia ambayo ni ya kipekee mintarafu ya lugha ya Ekegusii inavyotumika Goseta. Kwa mfano, utafiti uliwahi kunakili maumbo yanayotokana na lugha kama vile Kibukusu ambayo ni lugha ya jamii kubwa zaidi katika maeneo ya Trans Nzoia na pia kutoka lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha sambazi katika janibu hizi.

Kijamii, launi hii ya Ekegusii imeenea zaidi miongoni mwa vile vizazi vilivyozaliwa, kukulia na kusomea Trans Nzoia. Hivyo basi jambo hili linaifanya kuwa na sifa za lahaja ya kikundi mahsusi cha kijamii na hiki kwa mujibu wa uainishaji wao Aswani na wenziwe, ni kigezo mojawapo cha kuainisha lahaja.

7.1 Mapendekezo

Ingawa utafiti huu ulifaulu katika kuyaafikia malengo yaliyokusudiwa, kuliibuka na maswala mbali mbali yanayoweza kutajwa kama msingi wa kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

Pendekezo la kwanza ni kuwa huu ulikuwa utafiti wa kwanza wa jinsi hii kufanywa katika eneo hili kuhusu ubadilikaji wa lugha ya Ekegusii katika eneo la Goseta. Kuna haja ya utafiti zaidi hususan utakaolenga vipengele vingine vya lugha mathalani sintaksia na fonolojia ili kutoa picha kamili kuhusu kiwango cha ubadilikaji

wa lugha katika eneo hili.

Pili hamna lugha inayoselea katika hali ile ile moja daima. Mabadiliko tuliyoanakili basi hayawezi yakachukuliwa kama ndiyo mwisho wa kutokea kwa mabadiliko katika launi hii. Kuna haja ya utafiti katika uwanja huu kuendelea kwa minajili ya kurekodi hatima ya lugha ya Ekegusii hasa miongoni mwa watafitiwa wa kizazi cha sasa wanaosakini janibu zilizo mbali na Gusii.

Tatu ni kuwa yafaa hatua za mapema za uhifadhi lugha zitekelezwe na wadau husika ili kuzua mikakati ya kuzuia utowekaji wa lugha hii katika siku zijazo. Pendekezo hili linaongozwa na uvumbuzi tulioufanya uliodhihirisha kuwa lugha hii hutumika tu katika domeni haba ikilinganishwa na lugha za Kiswahili na Kiingereza.

Hatimaye, katika sura ya mwisho ya tasnifu hii, tulitaja uwezekano wa launi hii ya Ekegusii kutambulika kama lahaja ibuka ya lugha ya Ekegusii. Hata hivyo pana vigezo vingine vya uainishaji wa lahaja ambavyo hatukuvizingatia maadamu vilikuwa nje ya upeo wa utafiti huu. Kwa sababu hii, ni pendekezo letu kuwa utafiti zaidi ufanyike kuhusu launi kama hizi zinazotumika na wanajamii-lugha ya Abagusii wanaoishi nje ya maeneo ya asili ya Abagusii kama vile watafitiwa wetu wa Goseta.

MAREJELEO

Akama S.J (2006). *Gusii Demographic Trends ktk Akama S.J et al (Wah) Ethnography of the Gusii of Western Kenya: A Vanishing Cultural Heritage*. New York U.S.A: Edwin Mellen Press.

Anderson James.M (1986). *Structural Aspects of Language Change*. Essex, England: Longman Group.

Bally. C na Sechehaye (wah) (1966). *A Course in General Linguistics. Ferdinand De Saussure*. .New York U.S.A: McGraw-Hill.

Barber (2000) *.The English Language: A Historical Introduction* Cambridge U.K.: Cambridge University Press.

Bhat D.N.S (1999) *.The Prominence of Tense, Aspect and Mood*. Amsterdam,

Netherlands: John Benjamins.

- Buliba A, Njogu K na Mwihiaki A (2006) *.Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi, Kenya: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Cammenga J (2002). *Phonology and Morphology of Ekegusii: A Bantu Language Of Kenya*. Koln Germany: Rudiger Koppe Verlag.
- Cook V. (1997). *Inside Language*. New York U.S.A: Oxford University Press
- Crowley Terry (2000). *An Introduction to Historical Linguistics (3rd Ed)*. Auckland, New Zealand : Oxford University Press.
- Davies A.M. (1992). Comparative Historical Linguistics ktk Bright W. (mh) *The International Encyclopedia of Linguistics vol 2*. Oxford U.K.: Oxford University Press
- Dittmer Norbert (1976). *Sociolinguistics: A Critical Survey of Theory and Application*. London. U.K: Edward Arnold Ltd.
- Fishman J.A. (1972). *Language in Socio Cultural Change*. Standford ,U.S.A.: Standford University
- Hall J Christopher (1992). *Morphology and Mind. A Unified Approach to Explanation*
In Linguistics. London, U.K : Routledge .
- Hoenigswald H.M (1992). Historical Linguistics: Ancestry and Descent ktk Bright W (mh). *The international Encyclopedia of linguistics Vol 2*. Oxford U.K.: Oxford University Press.
- <http://www.thefreedictionary.com/morphology>*>morphology retrieved on 06/07/008
- <http://en.wikipedia.org/wiki/Morphology%28linguistics%29> .Retrieved on 05/07/008
- http://en.wikipedia.org/wiki/comparative_linguistics .Retrieved on 16/06/007
- <http://en.wikipedia.org/wiki/etymology>. Retrieved on 20/09/007
- <http://encarta.msn.com.1993-2005> Microsoft corporation: (2006).*Language. How language Changes*. Retrieved on 16/06/007
- Joseph D.B (1999). *Historical Linguistics*. Retrieved on 16/06/007 from <http://www.ling.ohio-state.edu/~bjoseph/publications/2001hist.pdf>
- Kamwangamalu M.N (2000).*Languages In Contact ktk Webb v. na Kembo-Sure (wah) African Voices. An Introduction to the Languages and Linguistic Of Africa*. Cape Town ,South Africa : Oxford University Press.
- Kembo-Sure and Webb. V (2000). *Linguistics: An OverView. Ktk Webb. V. na Kembo Sure (Wah) African Voices. An Introduction to the Languages and Linguistics of Africa*. Cape Town, South Africa: Oxford University press.

- Kimball E.S. (1992). *Comparative Method* ktk Bright W. (mh) *The International Encyclopedia of Linguistics* Vol. 2 Oxford, U.K.: Oxford University Press .
- Lodge. D (mh) (1988). *Ferdinand De Saussure Modern Criticism and Theory*. London, U.K.: Longman Group
- Massamba D.P.B (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar-es Salaam ,Tanzania: T.U.K.I.
- Massamba D.P.B. (2006). *Kiswahili cha Musoma; Mwanzo wa lahaja mpya Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchanguzi wa Kiswahili Juz # 69*. Dar es Salaam, Tanzania. T.U.K.I.
- Mathews P.H (1991). *Morphology (2nd Ed)* Cambridge U.K: Cambridge University Press.
- Mgullu R.S (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi, Kenya: Longhorn Publishers.
- Mohammed A.M na Mohammed S.A (2002). *Kamusi ya Visawe*. Nairobi, Kenya: East African Educational Publishers.
- Monari I.C. (2002). *Ekegusii for All Seasons*. Kisii, Kenya: Pangolin Books.
- Mugenda O.M na Mugenda A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi, Kenya: Acts Press.
- Mwaniki I.N. (2005). *Understanding Linguistics*. Nyeri, Kenya: Cetradin Press.
- Nettle D. (1998) .*Using Social Impact Theory to Simulate Language Change*. Retrieved on 17/08/2007 from <http://www.staff.ncl.ac.uk/daniel.nettle/lingual.pdf>
- Ochieng W.R. (1986). *People of The South Western Highlands: Gusii*. Nairobi, Kenya: Evans Brothers (K) Ltd
- Odeo I.I na Maina G. (2008). *Fani ya Isimu Jamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.
- Ogechi N.O.O (2006). *Language and Its Usage ktk Akama S.J n.w (wah) Ethnography of The Gusii of Western Kenya: A Vanishing Cultural Heritage*. New York, U.S.A : Edwin Mellen Press.
- Ogechi N.O. (1992). *Ubadilishaji Msimbo Miongoni Mwa Abagusii: Hali Halisi Katika Chuo Kikuu cha Moi na Kiamokama. Tasnifu Ya Uzamili (Haijachapishwa)* Eldoret, Kenya: Chuo Kikuu Cha Moi.
- Oso Y.W na Oneu O (2005). *A General Guide to Writing Proposals and Reports*. Kisumu, Kenya : Optians press..
- Sankoff G (2001). *Linguistic Outcomes of Language Contact Ktk Trudgill.P n.w (Wah) Handbook of Sociolinguistics*. Oxford U.K: Basil Blackwell .

- Sarantakos S. (2005). *Social Research 3rd Edition*. New York U.S.A.: Palgrave Macmillan.
- T.U.K.I. (2000). *English Swahili Dictionary 2nd Edition*. Dar es Salaam, Tanzania: T.U.K.I
- TU.K.I. (1981). *Kamusi Ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi, Kenya: Oxford University Press.
- Yule G (2000). *The Study of Language*. Cambridge U.K : Cambridge University Press.
- Were G.S. (mh) (1986). *Kisii District Socio Cultural Profile*. Nairobi, Kenya: Government Press .
- Ziegler A (1996). *Linguistics Theory, Foundations and Modern Development. An Overview of Linguistics and Linguistic Applications*. Retrieved on 17/08/007 from http://www.geocities.com/Athens/Acropolis_1470_shop_3_4_5.html linguistics theories. Foundations and modern development (1996)

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO 1: HOJAJI

BARNABAS .O .ABUGA,
 CHUO KIKUU CHA MOI,
 IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA,
 S.L.P 3900,
 ELDORET.

Kwa Bw/Bi

Mimi ni mwanafunzi wa uzamili katika idara ya Kiswahili ya chuo kikuu cha Moi Eldoret.

Ninafanya utafiti kuhusu mabadiliko katika lugha ya Ekegusii miongoni mwa wakaaji wa eneo la Goseta wilayani Trans Nzoia kwa madhumuni ya kuniwezesha kuhitimu shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili.

Ninaomba ushirikiane nami kwa kuyajibu maswali yafuatayo.

Mimi wako

Bw. Barnabas.O.Abuga

14. Iwapo ulifunzwa lugha ya Ekegusii rasmi, ulifunzwa hadi kiwango kipi?

- a) Shule ya msingi
- b) shule ya upili
- c) chuoni

15. Unaweza kuongea lugha zipi nyingine kati ya hizi

- a) Kiingereza: ndio la
- b) Kiswahili: ndio la
- c) Kibukusu: ndio la
- d) Kinandi: ndio la
- e) Kiturkana: ndio la

16. Unapokuwa katika mazingira yafuatayo wewe huongea lugha ya Ekegusii:

- a) **nyumbani**:kila mara wakati mwingine kwa nadra
- b) **sokoni**: kila mara wakati mwingine kwa nadra
- c) **mtaani** : kila mara wakati mwingine kwa nadra
- d) **kanisani**:kila mara wakati mwingine kwa nadra
- e) **Kazini**: kila mara wakati mwingine kwa nadra

17. Je wewe hutumia lugha ya Ekegusii katika shughuli zifuatazo?

- a) Kuandika barua : ndio la wakati mwingine
- b) Kusoma magazeti: ndio la wakati mwingine
- c) Kusikiza vipindi vya redio: ndio la wakati mwingine
- d) Kusali: ndio la wakati mwingine
- e) Unapozungumza na wazazi wako: ndio la wakati mwingine
- f) Unapozungumza na mkeo/mmeo: ndio la wakati mwingine
- g) Unapozungumza na wanao: ndio la wakati mwingine
- h) Unapozungumza na mahirimu wako Abagusii: ndio la
wakati mwingine

- i) Unapozungumza na chifu wa eneo hili: ndio la wakati mwingine
- j) Unapokutana na Abagusii majirani zako: ndio la wakati mwingine
18. Unadhani kuhamia kwa Abagusii Goseta kumechangia kubadilika pakubwa kwa lugha ya Ekegusii?
- Ndio
 - Si sana
 - La
 - sijui
19. Kwa jumla unaweza kusema kuwa lugha hii ya Ekegusii inakufaa katika shughuli zako zote za kimawasiliano hasa unapowasiliana na Abagusii wenzako:
- inanifaa kabisa
 - inanifaa kiasi
 - hainifai hata kidogo
20. Wewe hujihisi kuridhika na uwezo wako wa kuzungumza lugha ya Ekegusii?
- naridhika kabisa
 - Nimeridhika kwa kiasi tu
 - Siridhiki hata kidogo
21. Wawezaje kuukadiria ujuzi wako wa lugha ya Ekegusii katika viwango hivi:
- 0/10
 - 5/10
 - 10/10
22. Je ukipata fursa ya kujifunza lugha ya Ekegusii kwa minajili ya kuimarisha ujuzi wako utaichukua?
- Ndio b) la

Ahsante Kwa Muda Wako

KIAMBATISHO 2: DODOSO LA KWANZA

Utangulizi

Utafiti huu unalenga kuchunguza misamiati mbali mbali ya Ekegusii kwa lengo la kubainisha iwapo unaitambua na vile vile kupata maoni yako kuhusu hali ya lugha ya hii ya Ekegusii hapa Goseta.

1. Tafadhali nielezee dhana zifuatazo katika lugha ya Ekegusii?

1.1. Dhana zinazohusu mazingira :

- a) Anga
- b) Jua
- c) Giza
- d) Mawingu
- e) Masika
- f) Mvua ya rasharasha
- g) Gharika
- h) Ukungu
- i) Upepo
- j) Kiangazi

1.2. Majina ya wanyama wa kawaida wafuatao:

- a) Kuchakuro
- b) Swara
- c) Ndovu,
- d) Twiga,
- e) Kifaru
- f) Mbweha.
- g) Simba
- h) Tumbili
- i) Punda milia

j) Fisi

1.3. Wanyama hawa hufugwa nyumbani, je hujulikanaje katika lugha ya Ekegusii:

- i. Punda
- ii. Kondoo jike
- iii. Kondoo dume
- iv. Mbuzi dume
- v. Mbuzi Jike,
- vi. Ngombe Mweupe
- vii. Ngombe mweusi
- viii. Ngombe mwenye madoa
- ix. Ngombe wa rangi ya kijivujivu
- x. Maksai
- xi. Kongoro

1.4. Nyakati zifuatazo za siku zina majina maalum ya Ekegusii waweza kuyataja majina hayo?

- a) Asubuhi,
- b) Alfajiri,
- c) Machweo,
- d) Jioni

1.5. Tafadhali nitajie Siku za juma katika lugha ya Ekegusii

1.6. Nitajie majina ya miezi yo-yote mitano ya mwaka katika lugha ya Ekegusii

1.7. Nitajie idadi zifuatazo 1,5,8,12,27,59,70,84,98,100,103,110 katika lugha ya ekegusii

1.8. Unajua methali zo zote za Ekegusii? Iwapo wazijua, nitajie zo zote tatu.

2. Je wewe unaunga mkono dai ya kwamba kile kinachozua hisia kuwa kuna tofauti kati ya Ekegusii cha hapa na cha Gusii ni kule kuwepo kwa maneno mengi yasiyopatikana katika Ekegusii cha kule Gusii na ambayo yanapatikana katika kile cha hapa?

2.1.1. Iwapo unakubaliana na dai hili tafadhali nitajie baadhi ya maneno unayoyajua na ambayo yanaleta mtafaruku huu.

2.1.2. Unadhani nini ndicho chanzo cha hali hii.

3. Ni ugumu upi unaokumbana nao katika mawasiliano yako unapotumia lugha ya Ekegusii unapozungumuza na:

- 3.1.1. Wazee
- 3.1.2. Marika
- 3.1.3. Watoto wadogo

4. Kwa jumla unaweza kusema kuwa lugha hii inakutosheleza katika shughuli zako za kimawasiliano unapotagusana na Abagusii wenzako.
5. Je ungependelea wanao wajifunze lugha hii katika siku za usoni?

KIAMBATISHO 3: DODOSO LA PILI

Majina:

Umri:

Jinsia:

Anwani:

.....

.....

1. Wewe uliamia hapa ama ni mzawa wa hapa?

1.1. Iwapo wewe si mzawa wa hapa, ulizaliwa wapi? _____

1.2. Ulihamia hapa mwaka gani? _____

1.3. Ulipo hamia huku, ulihama pekee yako au ulikuwa mwanachama wa kundi maalum la wanunuzi wa mashamba? _____

1.3.1. Iwapo ulikuwa mwanachama wa kundi maalum, wanachama wenzako walitokea eneo moja la Gusii au ni maeneo tofauti _____

1.3.2. Tafadhali nifafanulie zaidi jibu lako _____

1.4. Ulipo hamia hapa idadi yenu ilikuwa ya watu wangapi? _____

1.5. Hivi sasa jee unaweza kukisia idadi ya wakazi wa eneo hili? _____

2. Je nyote muishio hapa Goseta mlitoka eneo moja kule Gusii ndipo mkahamia huku?

2.1. Iwapo mlitoka maeneo tofauti tafadhali nitajie maeneo hayo _____

2.2. Ni sababu zipi zilizokufanya wewe pamoja na wenzio kuhamia huku?

2.3. Je kuna Abagusii ambao bado wanahamia huku Goseta kutoka maeneo ya Gusii?

2.3.1. Je sababu zao za kuhama huku ni swa na zile zilizo wafanya kuhamia huku hapo awali? _____

2.3.2. tafadhali fafanua _____

3. Bado unadumisha uhusiano wa karibu na jamaa zako uliowaacha ulikotoka_____
 - 3.1. Mara ya mwisho kwako kwenda huko Gusii ilikuwa ni lini? _____
 - 3.2. Wewe huhudhuria shughuli kama vile za sherehe za arusi, mazishi na nyinginezo kule Gusii uhitajikapo?
 - 3.3. tafadhali fafania jibu lako zaidi_____

4. Je miongoni mwenu hapa Goseta kuna watu wa makabila tofauti na Abagusii? _____
 - 4.1. Iwapo wapo watu wa makabila tofauti, yataje makabila yao_____
 - 4.2. Je katika mashamba yanayopakana na hili lenu, mna watu wa makabila tofauti nanyi? _____
 - 4.3. Nitajie makabila yao_____
 - 4.4. Je kutagusana kwenu kama Abagusii na watu hawa wa makabila tofauti kumeathiri kwa vyo vyote lugha yenu _____
 - 4.5. Tafadhali nifafanulie zaidi _____

5. Inadaiwa kuwa lugha ya Ekegusii inavyozungumzwa hapa Goseta ni tofauti na inavyozungumzwa kule Gusii?
 - 5.1. Wewe unakubaliana na madai haya? _____
 - 5.2. tukizingatia kipengele cha maneno, tafadhali nipe mifano kuonyesha jinsi tofauti hizi zinavyojidhihirisha_____
 - 5.3. Kwa makisio yako ni nini kinacho sababisha tofauti hizi kuzuka? _____